# *Ushuhuda Wa Shahidi Wa Kweli*

Asante, Ndugu Neville, Bwana akubariki. Habari za asubuhi, marafiki. Ni majaliwa kurudi hapa katika nyumba ya Bwana, asubuhi ya leo, na kusimulia tena ile hadithi ya kale, ya kale sana ambayo tumesimulia miaka hii yote, kwa watu wengi, kwamba jinsi ambavyo neema ya Mungu imeonekana kwetu, kupitia Yesu Kristo.

2 Na nina furaha sana kujua leo hii ya kwamba tunashiriki neema hii kote ulimwenguni, pamoja na watu kila mahali, kujua ya kwamba Mungu ana watoto Wake kila mahali. Labda wakati mwingine hatuioni hasa katika mmoja kwa mwingine, kama vile tungefanya ama tunavyopaswa kufanya. Lakini kwa kawaida ikiwa ni katika wakati wa shida, hapo ndipo yote yanapokuwa dhahiri.

3 Na hilo ndilo moja la mawazo yangu asubuhi ya leo, ya kwamba singejua jinsi ya kuwaelezea ninyi watu, furaha na shukrani zangu kwenu, kwa yale mmetutendea, kama familia, katika wakati wetu wa shida na mahitaji. Ni Umilele tu utakaoweza kuninii. . .nitakapoweza kuwaelezea kile urafiki wenu mwaminifu ulichomaanisha kwetu katika wakati huu wa shida, kama vile kuondoka, kwenda Nyumbani kwa mama. Kamwe sikutambua kile kulichomaanisha, sana kama sasa, kama kile kilichomaanisha wakati mtu anapokuja kukuona wakati ukiwa mgonjwa.

4 Mara nyingi ambazo nimekabiliwa na shida hizo, za kupata miito mingi sana ambayo nisingeweza kuishughulikia, na nimewashirikisha wahudumu wengine miito yangu, wapate kunisaidia kuendelea. Ndipo ninatambua kwamba kidogo inasababisha kuvunjika moyo; kwa kuwa, labda huenda ikawa wamemwita mhudumu huyu mwingine, pia, bali walikuwa wameniita mimi nije. Basi linanifanya mimi kujisikia kama laiti ningalikuwa na nguvu nyingi kupita kiasi, kushughulikia kila mmoja wa hiyo.

5 Kwa kuwa ninajua, nilipowaita watu mbalimbali, jinsi ambavyo kila mmoja alikuja kwa wakati mzuri sana; na jinsi, kile hilo lilichomaanisha kwangu, kuwaona wakitokea. Na kwenu ninyi watu mlioketi usiku pamoja na mama, Dada Wilson hapa, na Ndugu Fred Sothmann na mke wake, na, loo, wengi sana wenu. Na wengi sana mlitoa usaidizi wenu ambao haikutubidi kuukubali, bali mlijitolea; wengi sana hata

kungekuwako na mtu, pamoja naye, wakibadilishana kila dakika chache. Mlikuwa wema sana.

6 Na katika wakati ambapo sisi tulikuwa. . . tulipomwacha kwenye nyumba ya kuhifadhi maiti, jinsi mlivyokuja na kututembelea, na kutupa mikono, na kutukumbatia, na kutupa rambirambi zenu. Kamwe sikujua hilo ni muhimu sana, mpaka liliponijia mimi. Maua, mashada na vikapu kutoka kila mahali, hata wasingeweza kuviweka kwenye ukumbi wa mazishi, iliwabidi kuviweka nyuma kwenye vyumba. Jinsi ambavyo. . . kamwe sikufikiri kwamba kutuma tu shada la maua kulikuwa muhimu sana, mpaka wakati huo.

7 Na wengi wenu mmetuma kadi kutoka mahali mbalimbali, na kusema. . . kadi za rambirambi, mkiweka fedha ndani yake za kusaidia kwenye matumizi na kadhalika. Kamwe sikutambua ya kwamba zawadi ndogo kwa mtu fulani ama kitu kidogo kama hicho kingekuwa na maana sana, mpaka jambo hilo liliponijia. Mungu awabariki sana daima!

8 Nina furaha sana kujua ya kwamba mimi ni sehemu ya watu walio na roho wa namna hii. Nina furaha sana kujua ya kwamba mimi ni ndugu yenu. Nami ninatumaini ya kwamba haitanibidi kamwe kuwalipa kwa njia hiyo, bali katika njia nyingine.

9 Ndipo mimi, nikiwa nimesimama kwenye nyumba ya kuhifadhi maiti, karibu na mama, na wengi sana wakiingia. Na watu wengine wanaoangalia kwenye, labda, huenda ikawa ni mtu wa rika langu, na kuushika mkono wangu na kusema, "Billy, imekuwa ni muda mrefu." Ningeangalia nyuma, nisingeweza kuwakumbuka, walikuwa wamebadilika sana. "Ulihubiri kwenye mazishi ya mtoto wangu mchanga. Ulihubiri kwenye mazishi ya mama yangu. Ulikuja kwangu, usiku wenye giza, baridi." Na, mambo hayo yote namna hiyo.

10 Linaelezea kweli Neno la mwanazaburi, ninaamini ndiye. "Kama mkate juu ya maji, itakurudia siku moja."

11 Na kama nilikuwa, nilikuwa na ufasaha wa kutosha, ama nilikuwa na kipaji cha kunena, ningetaka kumwambia tu kila mmoja wenu yale ninayowazia. Lakini si—siwezi kufanya hivyo kwa sababu si—sijui hata jinsi ya kulielezea. Lakini ninasema jambo hilo namna hii, ya kwamba, ninyi, kila mmoja, apate kujua ninayomaanisha. Ninawashukuru, kutoka kwenye vilindi vya moyo wangu.

12 Na jinsi ambavyo Maandiko yametimizwa, "Mchukuliane mizigo, na kuitimiliza hivyo sheria ya Kristo." Imekuwa ni ninii. . .

13 Kuondoka kwake kulikuwa ni jambo la kigeni kwangu. Na kamwe sikutambua kabisa ni kwa nini Roho Mtakatifu hakuniambia hapo kabla, kama nilivyoelezea mara ya mwisho nilipokuwa mimbarani hapa, kwenye asubuhi ile. Nao waliniambia ya kwamba alikuwa yuafa wakati huo, hospitalini.

Sikukubali hilo, kwa kuwa Yeye hakuwa ameniambia alikuwa anatuacha. Sasa, bila shaka, tunatambua jambo hili, ya kwamba kuna mambo mengi ambayo Yeye hufanya, anayoweza kufanya, na anafanya, yasiyombidi kutwambia lolote. Yeye hutuambia tu. . . Nami ninajua jambo hili moja, hata hivyo, ya kwamba Yeye hufanya yote yatende kazi kwa manufaa.

14 Na asubuhi ya leo, nilikuwa nimelala kitandani, nikiwazia jambo hilo: Wa kwanza kuondoka, katika familia yetu, alikuwa ni ndugu yangu, Edward. Nami nilikuwa huko Magharibi nikifanya kazi kwenye ranchi wakati alipotuacha. Sikuwa nyumbani, bali nilimwona, nikiwa bado ni mwenye dhambi, nilimwona kwa ono kabla hajaondoka.

15 Wa pili kuondoka alikuwa ni Charles. Nilikuwa. . . Aliondoka upesi, ghafla. Alikuwa. . . Nilikuwa nikihubiri huku chini kwenye lile kanisa dogo, la kipentekoste la watu weusi usiku huo, wakati Charles alipouawa kwenye barabara kuu, na gari.

16 Aliyefuata kutuacha alikuwa ni baba, akatuacha kwa ugonjwa wa moyo, alifia mikononi mwangu. Nikaikabidhi nafsi yake kwa Mungu; alituacha ghafla, upesi.

17 Aliyefuata kutuacha alikuwa ni Howard. Nilikuwa huko Magharibi likizoni, huko chini mtoni, Wa Kutokurudi, wakati ndege zilipoingia, zikaangusha miavuli midogo, ya kwamba, "Alikuwa ameondoka." Lakini mimi, bila shaka, nilimwona akituacha, miaka, miaka miwili ama mitatu kabla hajaondoka. Tulijua alikuwa anaondoka.

18 Bali mama amekuwa ndiye pekee aliyekawia. Nami nilifikiri labda hiyo ndiyo sababu Yeye hakuniambia. Hao wote walituacha kwa ghafla sana, mbona, Yeye. . . Wote walituacha kwa ghafla, isipokuwa mama. Yeye alikawia kwa muda wa majuma sita, majuma sita kamili.

19 Lakini huenda nikasema tu jambo hili, katika kulielezea. Shauku yangu ilikuwa ni kusimama karibu na mama yangu, na kuikabidhi nafsi yake kwa Mungu, wakati akiondoka. Kitu Fulani cha kigeni kilinipeleka hospitalini asubuhi hiyo, mimi na mke wangu. Naye alikuwa mahututi sana. Na jambo la mwisho ninaloweza kumkumbuka akifanya, wakati ningeweza—ningeweza kumwambia. Asingeweza kuzungumza. "Mama, ikiwa ungali unampenda Kristo, na Yeye anamaanisha kila kitu kwako, tikisa kichwa chako." Naye angekitikisa kichwa chake, nayo machozi yangetiririka usoni mwake. Yeye angali alimaanisha kila kitu, moja kwa moja kwenye mwisho wa safari. Nikampapasa shavuni, na kuuvuta uso wake kwa mikono yangu, na nikasema, "Mama, wewe ni askari halisi. Mimi ninakujivunia."

20 Nikawazia, "Sijui vile Shetani angalikuwa amesema, kama alivyofanya katika siku za Ayubu?" Mnajua, Mungu

hawezi kuyatwaa maisha yetu; inambidi Shetani afanye hivyo; tunaachiliwa tu kwa Shetani.

21 Na Shetani akijua jambo hilo, akijua ya kwamba wakati wake ulikuwa umewadia, akijua ya kwamba atatuacha, alimwambia Mungu, "Unajua, yeye ana mvulana ambaye ni mhubiri, watoto ambao wanakiri kwamba ni Wakristo. Acha nimtese tu kwa muda mfupi, nitawafanya wote wakukane."

22 La, kwa neema ya Mungu! Na jambo la mwisho aliloitikia kwa kichwa chake, kwamba Kristo alikuwa angali ni kila kitu kwake, wakati alipotuacha.

23 Nilipokuwa nikija nyumbani, niliwazia, "Vema, sininii . . . " Niliingia, nikasimama mle chumbani. Nikachukua Biblia, Biblia mpya. Ndipo nikasema, "Bwana, Wewe ni Mungu. Sininii . . . Haikubidi kuniambia ufanyalo. Bali nilishangaa tu kama ulinificha, sababu ya Wewe kufanya hivyo, kumchukua, je! ilikuwa (ni kusudi) nisivunjike moyo? Kama ndivyo, naomba unifariji kwa Neno Lako."

24 Nami nikalifanya, wajua, jinsi unavyoichukua Biblia na kuifungua tu namna *hiyo*. Nilichukua tu vidole vyangu na kuipitia, nikaifungua. Mathayo 9, herufi kubwa mno nyekundu zikijitokeza, "Yeye hajakufa, bali amelala." Unaona, ndicho kitu cha kwanza macho yangu yalichoona katika hayo Maandiko, wakati nilipoangalia.

25 Hilo, bila shaka, sasa, mimi siitumii Biblia kama Hirizi, mnajua. Kamwe hatufanyi hivyo. Lakini nilikuwa nimehuzunika sana wakati huo mimi, nikiamini Mungu aliniacha nione hilo. Kwa sababu, kilichofuata, kilithibitisha kwamba ni kweli.

Usiku huo, bila shaka, ulikuwa usiku wa masumbuko.

26 Na kesho yake asubuhi nilikuwa kwenye . . . niliamka. Ninafikiri ilikuwa ni karibu saa mbili, chumbani, saa mbili ama labda baadaye. Nilianza kuona watoto wakiingia, hao wakiwaleta watoto walemavu kutoka kila mahali. Ilionekana kana kwamba walienea upana wa kama urefu wa jengo la mji, na urefu wa kama majengo mawili ya mji, ya watoto wanaoteseka pekee. Kwenye upande wa kushoto na upande wa kulia, kulikuwa na watu walioketi, na kotekote, ilionekana kana kwamba ilikuwa ni huko juu. Na ilikuwa kwa namna fulani, uwanja wa michezo, uliotelemka kisha ukaja tena kwenye upande wa mwisho, kuwazuia watu walio nyuma kabisa kuninii . . . Kutokuona; wangeweza kuiangalia kwa mbele. Nilipokuwa nimesimama, huku nimevaa suti ya bluu, niliwazia, "Sasa hii ni ajabu. Ni—ninajua ninasimama chumbani nyumbani, lakini mimi huyu hapa nikiwa na suti ya bluu."

27 Nami nilikuwa nikiongoza uimbaji, "Waleteni, waleteni," nikifanya pande zote mbili ziimbe, "waleteni watoto wadogo kwa Yesu, waleteni kutoka kwenye ulimwengu wa dhambi."

28 Ndipo akatokea mama aliyejulikana sana akaingilia upande wa nyuma wa ule uwanja. Kwa namna moja, au nyingine, nilijua ya kwamba alikuwa anaingia. Lakini akaanza kuja kupitia kwa wasikilizaji.

29 Nami niliendelea tu kuongoza nyimbo na. . . "Waleteni!" Ningesema, "Upande *huu* uimbeni, 'Waleteni!' Upande *huu*, 'Waleteni,' namna hiyo, 'waleteni wanaotangatanga kwa Yesu.'"

30 Nami nilikuwa ninataka kuwaombea watoto hawa wote wadogo wanaoteseka, na ni wagonjwa.

31 Basi mama huyu akaja na kuenda kwenye kibanda, kama vile kwenye jumba la maonyesho, ambapo ni kama mahali ambapo watu mashuhuri wanaketi, ama kibanda cha Rais. Ama, mnajua ninachomaanisha, katika mahali pa namna hiyo, kwenye mkono wangu wa kushoto.

32 Mama huyo alikuwa ndiyo kwanza aingie. Akawageukia watu hao wengine waliokuwa pale, na akainamisha tu kichwa chake. Nikaona kidogo alikuwa amevaa kwa mtindo wa kale. Ndipo mama huyo akageuka apate kuniinamia, kabla tu. Nami nilikuwa basi nimekwenda mimbarani kuhubiri. Na wakati tu alipokiinamisha kichwa chake, ndipo nilipogeuka namna *hii*, kumwelekea.

33 Basi nilipoinua kichwa changu, naye akainua kichwa chake, akiniangalia, ilikuwa ni mama yangu. Naye akaniangalia, na kutabasamu. Alikuwa ni kijana, mchanga kweli. Ndipo Sauti kubwa sana ya ngurumo ikapatikisa mahali pale, na maneno yakatokea yakasema, "Usijisumbue juu yake, yeye yuko jinsi alivyokuwa katika mwaka wa 1906."

34 Na wakati hilo ono liliponiacha, niliangalia, kuona kile mwaka wa 1906 ulichokuwa. Huo ndio mwaka alipokuwa bibi-arusi wa baba yangu. Nami ni—ninajua sasa, pia, ya kwamba yeye ni sehemu ya Bibi-arusi, Bibi-arusi wa Yesu Kristo.

35 Daima nitamkosa mama yangu. Alikuwa mzuri sana na mpendwa kwetu sote. Ninaweza kukumbuka mikono yake mizee iliyokuwa inatetemeka, yenye ugonjwa wa kutetemeka mwili, wakati ilipombidi Delores kuutuliza mkono wake, papo hapo, apate kumpa ushirika wakati wa mwisho alipokuwa maskanini, mbali na wakati mazishi yake yalipohubiriwa.

36 Ninataka kusema jambo jingine. Na papo hapo wakati mama alipokuwa akituacha, ni ajabu, haibashiriki, hatukujua anatuacha wakati huo. Lakini Ndugu Neville aliingia. Mke wangu akasema, kama kuna wakati mmoja niliofurahia kumwona Ndugu Neville, ilikuwa ni wakati huo. Kasema. . . Sijui ni kwa nini, bali jambo fulani tu, jinsi tu Mungu anavyotenda mambo hayo! Ndugu Higginbotham alikuwa pale pia, yule aliyetoa ujumbe kitambo kidogo tu kilichopita, akaingia. . . akakaa kwenye mlango wa huo ukumbi. Ndipo Ndugu Neville akaingia. Nami nikawaweka watoto

kukizunguka kitanda, na nikasema, “Sasa hebu sote tukaribie, na tufanye . . . hebu Ndugu Neville.”

37 Mama daima alipenda kumsikia Ndugu Neville akiomba. Alipenda tu kumsikia. Kasema, “Alizungumza kama tu kwamba, kwa uaminifu, alikuwa akizungumza na Mungu.”

38 Hayo ndiyo ya mwisho aliyosikia masikioni mwake, Ndugu Neville alikuwa amesimama, anaomba. Nami nilikuwa nimeweka mikono yangu juu ya kichwa chake, na mmoja juu ya mkono wake, hapo alipokuwa akiomba. Na wakati alipokuwa katika maombi, Mungu akamwita. Nami nikahisi ule mkutuo mdogo, wa kipekee, ndipo nikaangalia kote. Alikuwa amekigeuza kichwa chake na kuniangalia, nami nilijua alikuwa anaondoka. Kwa hiyo nikasema, “Mwenyezi Mungu, ninaikabidhi nafsi yake Kwako sasa.” Naye akaninii . . . ni kama upepo ulipitia chumbani, ndipo akaondoka kwenda kukutana na Mungu. Kwa hiyo, siku moja yenye utukufu kwenye ng’ambo ya pili, nitamwona, msichana.

39 Bila shaka, tunamjua sasa kama mama mzee aliyeugua, anayetetemeka. Wakati alipowazaa watoto wake, hao kumi, haikuwa ni kama tunavyofanya siku hizi. Hatukuwa na njia za kisasa, wala hatukuwa na fedha za kulipia. Mama angemzaa mtoto wake, tuseme, asubuhi ya leo, na alasiri ya leo angefua nguo zake. Na jambo hilo lilimdhoofisha.

40 Bali hatakuwa mama mzee anayetetemeka kwa ugonjwa wa kutetemeka, bali atakuwa ni msichana mrembo katika ule Ufalme wa huko ng’ambo.

41 Nami niliwazia juu ya faraja ya Mungu, kuniruhusu nifikie wakati huo. Halafu mara baada ya hayo yote kwisha, ndipo aniambie sababu yake. Kisha anipe hayo maneno ya faraja, kwa ono la mama yangu.

42 Kwa hiyo, enyi marafiki, Injili ambayo nimeishindania, nimeiangalia wakati inapofikia kwenye nyakati za mauti. Nimeiona kwa mama yangu. Nimeiona kwa mke wangu. Nimeiona kwa ndugu zangu. Ni—ninajua inachomaanisha unapofikia kwenye mwisho wa safari yako, ukiwa na tukio na Mungu. Inamaanisha jambo fulani. Kwa hiyo sasa nimeyakinia, kwa neema ya Mungu, kwenda katika kila sehemu ya ulimwengu, ambako Yeye atanipeleka, kwa kila kiumbe niwezacho, na kuihubiri Injili hii, kwa maana ni Nguvu za Mungu, kwa wokovu.

43 Nikijua jambo hili, ya kwamba wakati maisha haya yatakapokwisha, tunayo maisha ng’ambo ya pili, ambapo tutabadilishwa kuwa vijana tena, nasi tutaishi katika Uwepo Wake na baraka Zake, milele na milele. Ninatumaini ya kwamba kila mama wa thamani aliye hapa ndani, na kila binti, kila mwana, na kila baba, atakufa katika Bwana. “Hata hivyo asema Roho; kwa kuwa wanapumzika kutokana na kazi zao,

na matendo yao yanawafuata." Siku moja angavu tutaenda na kuwaona! Naam.

44 Kama hivyo sivyo, basi mbona tunasimama hapa asubuhi ya leo, tukihubiri bure? Lakini, enyi marafiki, dini yetu si bure. Ni Nguvu za Mungu, zilizojaribiwa moja kwa moja kwa majaribio makali sana ya mauti. Kwa mateso, kwa njia yoyote yanayotaka kupitia, inaleta tofauti gani? Tunaenda kukutana na Mungu.

Sasa ninapenda kuninii . . . nilikuwa . . . tulikuwa na viti kwa ajili ya kila mtu.

45 Nami ninataka kutangaza, ninaamini usiku wa leo ni ushirika. Hiyo ni kweli, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Usiku wa leo ni usiku wa ushirika. Na kila mtu kwenye . . .

46 Niliwazia tu, jambo fulani kuhusu ushirika. Kulikuwako na mtu fulani, hivi majuzi, aliyeenda kanisani, na ilimbidi kuchukua teksi impeleke kanisani. Yeye ni maskini hohehahe. Basi akashuka akaenda kula ushirika, naye jirani yake kwa namna fulani ni . . . loo, kwa namna fulani ni mmoja wa hao jamaa wakaidi wasiomjua Mungu. Naye alimuuliza jirani yake, akasema, "Ulienda wapi asubuhi ya leo, kwa ile teksi?"

47 Kasema, "Nilifikiri . . ." Yeye, mtu huyo, ni vigumu kupata chakula mezani mwake. Akasema, "Kanisa linafanya ushirika, kwa hiyo nilishuka kwenda kula ushirika."

Akasema, "Kwani ushirika ni kitu gani?"

Akamwambia ulikuwa ni nini, "Mkate na divai ya Bwana."

48 Akasema, "Nami nilikula, pia." Kasema, "Nilikuwa na karai nzima ya biskuti na kisaga cha wiski." Na akiwa mezani mwake, papo hapo, akashikwa na mshtuko wa moyo. Wanamtazamia kuaga dunia dakika yoyote. Usiwe mkufuru. Usikose kicho. Unaona? Liheshimu Neno la Bwana, unaona, kwa maana hatujui ni dakika gani tutakapoitwa kwenda kuwajibika, na, kwa Mungu.

49 [Mtu fulani anasema, "Je! utakuwa hapa usiku wa leo?"—Mh.] Sasa samahani. ["Utakuwa hapa usiku wa leo?"] Ninadhamiria kuja. Ndiyo. Waliniuliza iwapo nitakuwa hapa usiku wa leo. Ninadhamiria kumsikia mhubiri mzuri usiku wa leo, nikiweza, Ndugu Neville. Lakini, ninadhamiria kuja katika kila usiku wa ushirika. Nafikiri ni majukumu yetu, kadiri tuwezavyo.

50 Basi kama ni sawa, kama inampendeza Mungu, na inalipendeza kanisa na Ndugu Neville, ninataka kuwa hapa Jumapili ijayo, tena, Bwana akipenda. [Ndugu Neville anasema, "Amina!"—Mh.] Na kama ni sawa, unaona. ["Loo, amina! Naam."]

51 Na ni—ninafikiri tu ya kwamba ninataka kutoa kila wakia mdogo niwezao, kila chembe ya nguvu zilizosalia, kwa ajili ya

Ufalme wa Mungu; kila kitu, kuokoa kila nafsi ninayojua jinsi ya kuiokoa. Kwa sababu, hata hivyo, ni—ningefanyaje asubuhi ya leo kama mama asingekuwa ni Mkristo, kama hatukuwa na lile tumaini lililobarikiwa la ng'ambo ya pili? Kama mimi . . .

52 Ninakumbuka, moja kwa moja chini ya nyumba yangu, nilimbatiza, miaka thelathini na moja iliyopita, katika Jina la Yesu Kristo; chini tu ya nyumba yangu, pale mtoni. Ninaweza tu kumwona akija sasa, na kunikumbatia. Hilo lilimaanisha mengi sana. Nikasema, "Mama, siku moja tutakuweka katika kaburi la matope." Nikasema, "Lakini yeye aaminiye, na kubatizwa, ataokolewa." Hilo ni . . . Naam.

53 Na kwa hiyo kama sikuwa nimeileta nafsi yoyote nyingine kwa Mungu, mbali na hiyo ya mama yangu, kila jitihada imelipiwa mara milioni moja. Naam. Naam, bwana. Hiyo ni kweli.

54 Sasa kwa somo la Maandiko, ninayo Maandiko mawili. Kwa hiyo ninataka kusoma moja la hayo kwanza, kisha tutaomba, halafu ninataka kusoma hayo mengine. Nanyi ambao mngetaka kusoma pamoja na mimi, fungueni Biblia zenu kwenye mlango wa kwanza wa Matendo. Nami ningetaka kutangaza somo langu, asubuhi ya leo, Bwana akipenda. Sasa, sababu . . . Nina Maandiko mengi na muhtasari hapa ya kuzungumzia. Sitajaribu kuwaweka kwa muda mrefu sana.

55 Lakini mimi ninajaribu kusoma, kuketi chumbani. Na kama Bwana hanipi chochote, ambacho ninafikiri kinafaa . . .

56 Ninataka kusanyiko hili na wote wajue. Sishuki kuja huku nipate tu kuonekana. Ninashuka kuja hapa, si kwa sababu tunahitaji mhudumu. Kwa sababu, ninafikiri mchungaji wetu ni mmoja wa walio bora sana nchini. Hiyo ni kweli kabisa. Si hivyo.

57 Lakini, ninakuja kwa sababu ninajisikia ya kwamba Mungu ameweka moyoni mwangu Ujumbe ambao utawasaidia watu hawa. Mnaona, kitu fulani ambacho kitawasaidia. Na sote pamoja, tukiwa na mchungaji wetu wa thamani, sote wawili tukiongozwa na Roho Mtakatifu, tunaweka wakati wetu pamoja, na kuuchunga, ili kumwokoa kila mtu tuwezaye. Nami nimekuja asubuhi ya leo, kwa sababu nilijisikia ya kwamba Roho Mtakatifu alinipa, Ujumbe ambao ungeweza kulisaidia kanisa. Na hiyo ndiyo sababu mimi nipo hapa.

58 Sasa katika mlango wa kwanza wa Kitabu cha Matendo, tunaanza kusoma kwenye kifungu cha 1.

> *Kitabu kile cha kwanza nalikiandika, Theofilo, katika habari za mambo yote aliyoanza Yesu . . . kufanya na kufundisha;*
>
> *Hata siku ile alipochukuliwa juu, alipokuwa amekwisha . . . kuwaagiza kwa Roho Mtakatifu wale mitume aliowachagua;*

> *Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi zisizokanushika, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena. . . mambo yaliyouhusu ufalme wa Mungu.*
>
> *Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalemu, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu;*
>
> *Ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache.*
>
> *Basi walipokutanika, wakamwuliza,. . . wakisema, Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?*
>
> *Akawaambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe.*
>
> *Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia. . . juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika. . . Uyahudi, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.*
>
> *Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao.*
>
> *Walipokuwa* wakikaza *macho kuelekea mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe,*
>
> *Wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona* ninyi *mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni.*

59 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu, kwa ajili ya maombi.

60 Baba yetu wa Mbinguni, sasa tunakuja tukikaribia, katika Jina la Bwana Yesu, kutoa mbele Zako, kwanza shukrani zetu kwa yale uliyotufanyia; na kwa ajili, zaidi ya yote, ile dhamana iliyobarikiwa ambayo imetulia mioyoni mwetu, ya kwamba sisi tumeokolewa; tumeokolewa kutokana na mauti, tumeokolewa kutoka kuzimu, tumeokolewa kutoka kwenye maisha ya dhambi, tumeokolewa kutoka kwa mambo ya ulimwengu, na tumeitwa kwenye ile Karamu Kuu ya Arusi ya Mwana wa Mungu. Jinsi tunavyokupenda, Bwana, kwa ajili ya jambo hili! Ni zaidi ya uhai kwetu; ni Uzima wa Milele!

61 Na tumekusanyika asubuhi ya leo, Bwana, kutoa masimulizi haya katika nyimbo, shukrani, na katika kuhubiriwa kwa Neno, kuwapa hao Neno la Uzima, Bwana, huenda wakawa hapa, wasiokujua Wewe. Na ni shauku yetu, na lengo letu na azma yetu, ya kwamba Hili leo litasababisha wengi, wasiokujua Wewe,

kuja na kukiri dhambi zao, na kuliitia Jina la Bwana, na kuondolewa dhambi zao, kwa kukiri dhambi zao na kubatizwa, kuosha dhambi yao. Na halafu, Baba, tungeomba ya kwamba utamjaza kila mmoja na Roho Mtakatifu, kwa kuwa Ndiye Muhuri wa ahadi ambayo Mungu ametupa.

62 Tungeomba ya kwamba ungewakumbuka wote walio wagonjwa na wanaoteseka na wahitaji, leo. Kwa maana ulimwengu kweli umo katika hali ya uhitaji, yote kwa sababu hatuji Kwako kwa ajili ya ulinzi wetu na kimbilio.

63 Jinsi tunavyoweza kuwazia, asubuhi ya leo, juu ya nyakati katika Biblia, wakati watu walipokuwa katika taabu na dhiki, jinsi walivyowaita manabii, na wengi wa hao watu wakuu katika siku hizo, walidhani hao manabii kwamba ni waliochanganyikiwa na—na watu wenye mfadhaiko wa akili. Na, ambavyo, huenda walikuwa hivyo, lakini hata hivyo walikuwa na Neno la Bwana. Mungu, leo hii, jinsi tunavyopaswa kurejea kwenye Neno la Mungu. Wametwambia kuhusu wakati wa mwisho, na yale yatakayotukia. Basi tujalie, kama Wakristo halisi, tuangalie ushuhuda wa—wao, na, Baba, ndipo tuushuhudie ulimwengu. Tujalie, Bwana.

64 Waponye wagonjwa walio miongoni mwetu asubuhi ya leo. Kwa kuwa tunatambua, Bwana, ya kwamba mwili mgonjwa, mchovu, uliochoka, unaokokotwa kila mahali, hauwezi kufurahia baraka za Mungu kama vile wangalizifurahia kama wangalikuwa ni wazima. Nasi tunatambua, kama Wakristo, ya kwamba tunaishi mbali sana na majaliwa yetu. Ya kwamba, Wewe hututaki tuwe namna hiyo, wachovu na waliochoka, na kuishiwa na nguvu na kuwa wanyonge. Unatutaka tujazwe na Roho wa Mungu. Tujalie hayo, Bwana, tunapoendelea kuungojea Ujumbe Wako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

65 Sasa, kama mtafungua tena kwenye Neno, katika Yohana Mtakatifu 3. Ninataka kusoma vifungu vichache kutoka katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 3, kuanzia kifungu cha 31, kama vifungu vitatu vya hili, tupate fungu dogo la yale ninayotaka kusema. Huyu ni Yesu akinena, Yohana Mtakatifu 3:31. Basi sikilizeni Neno Lake kwa makini.

> *Yeye ajaye kutoka juu, huyo yu juu ya yote. Yeye aliye wa dunia, asili yake ni ya dunia, naye anena mambo ya duniani. Yeye ajaye kutoka mbinguni yu juu ya yote.*
>
> *Yale aliyoyaona na kuyasikia ndiyo anayoyashuhudia, wala hakuna* anayeukubali *ushuhuda wake.*
>
> *Yeye aliyeukubali ushuhuda wake ametia muhuri ya kwamba Mungu ni kweli.*

66 Ningetaka kusoma kifungu hicho cha 33 tena, kutilia mkazo hicho kifungu cha 33.

*Yeye aliyeukubali ushuhuda wake ametia muhuri ya kwamba Mungu ni kweli.*

67 Kwa ajili ya somo asubuhi ya leo, kama mkininii . . . ninataka kutumia hili, *Ushuhuda Wa Shahidi Wa Kweli*. Ushuhuda na ushahidi! Hiyo ndiyo sababu nilisoma Maandiko hayo mawili tofauti, moja la ushuhuda na lingine la ushahidi.

68 Sasa, ushuhuda. Kabla . . . Mtu hana budi kuwa na tukio kabla hawajaweza kushuhudia. Kama uliitwa mahakamani, ungepaswa, kama, kutoa ushuhuda. Unapaswa kujua jambo fulani kabla hujashuhudia.

69 Na shahidi ni mtu ambaye ameona kitu fulani, ambaye anajua ya kwamba ni kweli. Nao wanaitwa kutoa ushuhuda. Halafu, basi, shahidi hana budi kujua yale anayozungumzia. Hapaswi kuwa, "Mtu fulani aliniambia jambo fulani." Hana budi kuwa shahidi, yeye mwenyewe. La sivyo, ananena habari za mwingine ambaye angeweza kuwa shahidi kwenye eneo la matukio.

70 Sasa, nafikiri ya kwamba, kwa kuwa tunaona kutoka kwenye kusanyiko letu, ya kwamba maisha ni dhaifu sana, basi, ya kwamba mauti ni halisi sana, tunapaswa kufikia mahali ambapo sisi tuna hakika kabisa ya kwamba Hili tunalonena habari zake ni kweli. Mnaona? Si kitu unachoweza kufanya shaghalabaghala, kama tusemavyo, kulikubali. Unapaswa kuwa na uhakika kabisa ya kwamba Hilo ni kweli, kwa maana hatujui tutafikia mwisho wa namna gani.

71 Sasa, sababu yenyewe ya mimi kuwa mwenye mawazo ya Kikalvini, ya usalama wa mwaminio, ni kwa sababu kwamba, ninaamini, ya kwamba wakati mwanamume ama mwanamke ana akili timamu, huo ndio wakati wa kumkubali Bwana Yesu. Na kuyatatua mambo yote wakati huo, mara moja daima. Kwa sababu, tutakapofikia mwisho wa safari yetu, hatujui ni wapi ama ni jinsi gani tutakavyokuwa wagonjwa. Huenda tukawa wagonjwa akilini mwetu, huenda kukawa na homa ambayo kweli itaathiri ubongo wetu hasa, na huenda tukasema lolote ama kufanya lolote mwishoni mwa safari. Hatujui. Lakini, mnaona, kama tayari tumetia nanga katika Kristo, haidhuru ni ugonjwa gani utakaotuchukua, ama tuko katika hali gani tutakapoondoka, yote yamekwisha.

72 Tumetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wetu. Waefeso 4:30, inasema, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku," si ya kufa kwenu, bali "ya ukombozi wenu." Mnaona, baada ya mauti kutokea, ungali umetiwa muhuri.

73 Sasa, kutoa ushuhuda, kumekuwako na mambo mengi na maswali mengi mioyoni mwa watu, na kumekuwako katika wangu.

74 Niliposimama majuma machache yaliyopita, wakati mama yangu alikuwa angali hai, na angeweza kusikia, nilikuwa upande mmoja wa kitanda, na dada yangu akisimama karibu na mimi. Ndipo mama akaangalia juu, akasema, "Wangu wa kwanza na wangu wa mwisho." Mimi ni kifungua mimba chake, Delores ni kitinda mimba. Pakiwepo na wavulana tisa katikati... Ama, kuna wavulana tisa na huyo msichana. Ndipo mama akaanza kusema, "Bill, umenilisha." Na kwa sababu, nadhani, nikiwa katika huduma, nilikuwa nina uwezo zaidi wa kufanya jambo hilo. "Na umenishughulikia. Na, Delores, ulinipenda na—na kunisaidia katika kazi yangu ya nyumbani na kufua nguo." Kisha kasema, "Halafu, Bill, uliniongoza kwa Kristo na umenitunza, kiroho. Na wakati nilipokosea, hukusita kuniambia ya kwamba nilikuwa nimekosea, na—na kwamba sina budi kulisahihisha."

75 Nami nikasema, "Na, mama, tumeninii..." Baadhi ya hao wavulana hunywa pombe. Na nikasema, "Tuliuvunja moyo wako."

76 Na, kama upendo wa mama, akasema, "Billy, hayo yote yanasaidia kuunda lile gurudumu kubwa."

77 Nikasema, "Mama." Yeye alijua asingerudi nyumbani, ama alisema asingerudi, kurudu kule Maple 409. Basi akaniambia... Nikasema, "Mama, nilipokuwa mvulana mdogo tu, nilijua ya kwamba kulikuwako na Mungu, kwa sababu nilikuwa nimeuona Utu Wake katika sura mbalimbali." Ndipo nikasema, "Mimi... Kwanza, mimi..." Nikiwa katika familia yetu, na tuliishi karibu na Bw. Wathen huko Utica Pike, na hatukujua lolote kuhusu kanisa. Wao walikuwa ni Wakatoliki.

78 Ndipo nikasema, "Nilianza kuchunguza. Sasa, kama vile kanisa Katoliki lisemavyo kwamba, 'Mungu alilipa kanisa Lake Nguvu Zake kuu, na akaliambia kanisa Lake, sana sana likiwa ni mwili wa waaminio, "Lolote mfanyalo, ni sawa."'" Ndipo nikasema, "Basi kama...nilichunguza hilo. Ndipo nikaanza kuona kuna makundi karibu mia tisa ya madhehebu ya waaminio. Basi kama Mungu alilikabidhi kanisa Lake mamlaka Yake, na kuwaambia, 'Lipuuzeni tu Neno hili. Hamlihitaji, hilo ni historia tu. Na—na kisha mnaenda na kulifanya, na lolote mtakalosema litakuwa ni sawa; si Biblia, bali ni kanisa, lolote kanisa lilisema.' Mama, nisingeweza kuweka msingi imani yoyote. Kwa sababu, kanisa Katoliki linasema jambo *moja*. Kanisa la Kilutheri linasema 'Ni *hivi*.' Kanisa la Kimethodisti lilisema, 'La, wote wamekosea. Ni *hivi*.' Kanisa la Kibaptisti linasema 'Ni vinginevyo.' Na imani mia tisa mbalimbali, nisingewekea msingi imani yoyote juu ya jambo hilo."

79 Lakini nikasema, "Nililofanya, mama, nilirudi nyuma nikasoma Biblia. Nami nikaifundisha vile vile hasa hao mitume waliifundisha. Sikubadili jambo moja. Waliposema 'ubatizo

katika jina la Yesu Kristo,' nilisema 'ubatizo katika Jina la Yesu Kristo'! Waliposema 'ubatizo wa Roho Mtakatifu,' nilisema 'ubatizo wa Roho Mtakatifu'! Nami nikaufundisha jinsi tu walivyoufundisha. Mama, nilipata matokeo yale yale waliyopata! Na ninaona Mungu yeye yule anayetokana na mafundisho yao, ni Mungu yeye yule anayekuja katikati yetu na kufanya mambo yale yale aliyowafanyia kule nyuma. Yeye hutufanyia siku hizi. Kwa hiyo, ahadi Yake ni, 'Yeye aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu yuna Uzima wa milele, Nami nitamfufua tena katika siku za mwisho.'"

Neno ni ushuhuda wa Mungu.

80 Kuna mashahidi wengine tungeweza kuwaita, asubuhi ya leo. Mmoja wao, hebu tuwazie juu ya mti. Ni majira ya mapukutiko, na wakati majira ya kupukutika majani umewadia sasa. Na tuchukue jani, hilo ni kama uhai. Nasi ni, kama tumezaliwa mara ya pili, sisi ni jani katika ule Mti wa Uzima.

81 Na mti huu ambao tunauona hapa nje mwituni, uhai hatimaye huondoka, unaondoka kwenye jani, kwa maana majira ya jani yamekwisha. Ndipo uhai huo unaliacha hilo jani, nalo jani litaanguka wakati uhai unapoliacha. Sisi sote tuna hakika kabisa juu ya jambo hilo, tunapoliangalia kutoka kwenye madirisha yetu sasa. Kwamba, mara uhai unapoliacha hilo jani, hilo jani litaanguka.

Na huo ndio ule mwili tunaouzika.

82 Lakini uhai uliokuwamo kwenye jani hilo, unarudi mahali ulipotoka, unashuka chini katika huo mti, hata kwenye mzizi. Na hapo unabaki kwenye mzizi wa mti, mpaka kwenye majira mengine. Kwa majira haya, jua limejiondoa, ama dunia imejiondoa kwenye jua, na inafuata m—mzingo inapozunguka; na iko mbali sana, na hali ya baridi inaelekea duniani. Kwa hiyo mzizi, unashikilia huo uhai wa jani hilo mpaka dunia itakaporudi tena, ndipo basi hakuna njia ya kulificha jani hilo lisirudi tena. Litarudi hakika tu kama vile jua linavyorudi! Litarudi. Lakini halina budi kungojea msimu mwingine, kabla halijarudi.

83 Na leo hii jambo hilo linatupa ushuhuda mkuu, kama shahidi wa Mungu wa maumbile. Kwa sababu, kwamba wakati tunapokuwa katika majira ya maisha ya kibinadamu, tukiwalea watoto wetu, tukioa na kuzikuza familia, haya ni maisha ama ni msimu wa maisha ya kibinadamu. Lakini wakati tumezaliwa kutoka Juu, mwili unarudi mavumbini mahali ulipotoka, na roho inashuka inaenda mahali ilipotoka, ama inapaa juu, hasa, mahali ilipotoka, kwa Mungu aliyeitoa, na majira mengine yatakuja. Na majira hayo, ambayo yatakuja, yatakuwa ni majira yasiyo na mauti. Na wakati Mwana wa Mungu anapowazukia na uponyaji katika mbawa Zake, itakuwa haiwezekani kabisa kuishikilia miili hiyo ardhini tena. Watafufuka katika uangavu

wa Mwana wa Mungu. Maumbile yenyewe yanashuhudia jambo hilo.

84 Kwa hiyo kama sisi ni Wakristo, na tumezaliwa kwa Roho, mauti hayawezi kushikilia kitu ila ushindi kwetu, kwa sababu maskini mwili huu uharibikao, ambao Shetani, angali na mamlaka juu yake, utaanguka katika mavumbi ya nchi. Bali wakati msimu huo! Huu ni msimu mwingine sasa; huu ni msimu wa kupatikana na mauti. Lakini msimu wa kutopatikana na mauti unakuja wakati Yeye asiyepatikana na mauti atakapokuja. Yeye atakuja pamoja na zile roho zisizopatikana na mauti ambazo zimerudi Kwake, kutoka duniani, nao watafufuka tena katika ule ufufuo, kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu, nao watanawiri katika Utukufu Wake.

Kila kitu duniani kinatoa ushuhuda.

85 Jua linachomoza Mashariki, kuonyesha mwanzo wa uhai; linapanda na kutua jioni. Asubuhi, ndege wanaamka na kuimba, na wanafurahi, tunajisikia wapya; jioni, tumechoka wakati jua linapotua. Linatoa ushuhuda ya kwamba kuna uhai na mauti; siku ilizaliwa, siku imekufa.

86 Mti uliishi, majani yalipukutika. Mungu alihifadhi, kwenye mizizi ya mti huo, ambapo uhai huu ulianzia, mahali ulipoanzia, chini katika mizizi, ninii...ukaondoka ukaenda ukafanya majani kwa ajili ya kivuli, unarudi tena mahali ulipotoka. Kupumzika tu, upate kuja katika msimu mwingine.

87 Uhai katika ua dogo, unaoanguka kutoka kwenye mbegu, unarudi mahali fulani tusipopajua. Lakini nyama yote huenda ikatoka kwenye hiyo mbegu, nayo mbegu iozee ardhini. Lakini hata hivyo kuna uhai mle ndani, ambao umefichwa kwa ajili ya ufufuo tena.

Kila kitu kinazungumza juu ya ninii, kinatoa ushuhuda.

88 Sasa, nimekuwa na majaliwa ya kusafiri sana kote ulimwenguni. Nami nimesikia dini mbalimbali. Nimesikia maoni mbalimbali. Nimewasikia Waislamu, Wabudha, na Makalasinga, Wajaini, na, loo, mamia mengi ya maoni mbalimbali ya dini, miungu, miungu wa kike, na mambo hayo yote. Lakini hakuna mmoja wao, si hata mmoja wao, hakuna hata mmoja wao aliye na chembe ya Ukweli juu yake!

89 Dini hii ya Kikristo ndiyo dini ya kweli; kifo, kuzikwa, na kufufuka. Maumbile yote, mbingu yenyewe, na dunia, zinashuhudia hilo. Ni shahidi wa Mungu kwa watu Wake, kila siku, ya kwamba kuna kifo, kuzikwa, na kufufuka. Kila msimu unaopita juu ya vichwa vyetu; tunaona mauti, kuzikwa, na kufufuka. Kwa hiyo, tunajua ya kwamba hii ni Kweli. Ukristo, kimsingi, ni Kweli. Unatoa ushuhuda wake.

90 Na inaonyesha ya kwamba ulifanywa na aliye mkuu, Mwenye Akili nyingi kabisa, kutimiza kusudi fulani. Uko hapa kwa kusudi fulani. Haikumbidi Mungu kufanya miti jinsi hiyo. Aliifanya namna hiyo, ingawa inatofautiana, mmoja na mwingine, na kadhalika. Aliifanya hiyo yote kwa kusudi Lake, kutoa ushahidi na kushuhudia. Angeliweza kuifanya miti kama kitu ambacho kinge—kingekuwa kitu kingine, kama miamba. Angeliweza kuifanya miti vyovyote alivyotaka. Angeliweza kufanya maua vyovyote alivyotaka. Bali aliyafanya yapate kutoa ushuhuda, kwa kuwa hayo ni mashahidi wa Mungu. Ni mashahidi wa kweli, ya kwamba dini zingine zote ni za uongo, na Yesu Kristo ni mkweli. Kifo, kuzikwa, na kufufuka, vinatoa ushuhuda ya kwamba hatufi Milele, bali tunaishi tena. Inaonyesha Mwenye akili nyingi kabisa!

91 Huenda sisi, kama wakati ukiruhusu. . .Ambao, hatutaki kuchukua muda mrefu sana. Lakini huenda tukazungumza tena. . .Na, si kujilinganisha. Hii ni Maskani ambapo sisi tuna Maonyo yetu wenyewe na Mafundisho, na hapa ndipo mahali ambapo ninaweza kufundisha yale ninayowazia ni kweli.

92 Ninataka kuangalia Mwenye akili mwingine, tukinena juu ya neema ya Mungu ambayo imetuzukia. Je! ulitambua, kitu cha kwanza ni mzizi, kitu cha pili ni shina, kitu cha tatu ni tunda, na hilo linaumalizia.

93 Kuhesabiwa haki, mzizi; kutakaswa, shina; nalo tunda, Mbegu ya asili. Na hao ni Martin Luther, John Wesley, na ubatizo wa Roho Mtakatifu; kuhesabiwa haki, kutakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Huo unatoa ushuhuda wa maoni yetu juu ya Maandiko. Nami nina vitu dazani moja vilivyoandikwa papa hapa, ambavyo ningeweza kusema juu ya jambo hilo, hilo, juu ya vitu mbalimbali vinavyotoa ushuhuda. Kwa kuangalia vitu vya kawaida, vinatoa ushuhuda juu ya mambo ya kiroho. Kuhesabiwa haki, mizizi; kutakaswa, shina; na ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunda linalozaliwa kutokana na matokeo ya mzizi na shina.

94 Mzizi huo ulitoka kwenye mbegu. Mbegu ilikuwa kama ile iliyoingia ardhini, imerudi tena.

95 Na leo hii: tumeishi kupitia katika wakati wa Luther, tuliishi kupitia wakati wa Wesley, na sasa tunaishi katika wakati wa Waliokombolewa, wa kipentekoste. Ni kitu gani? Kurudisha Kanisa lile lile, kitu kile kile kilichopandwa kwenye Siku ya Pentekoste. Maumbile yenyewe yanatoa ushuhuda kwake; jinsi ile ile yanavyotoa ushuhuda wa kifo, kuzikwa, na kufufuka.

96 Loo, kwa Mungu wa Milele, na kwa shuhuda Zake! Laiti tungaliweza tu kuangalia kila mahali, ungemwona Mungu kila mahali, tukimwangalia akishuhudia kila siku. Tunakwazikaje makusudi, kijinga, juu ya mambo hayo, urahisi huo? Mbona, kila mti unatuhubiria. Kila ua linatuhubiria.

Kila bustani inatuhubiria. Ulimwengu mzima unatuhubiria. Mungu ni Mungu, nasi tunauona Utukufu Wake. Na hata hivyo tunakwazika makusudi sana juu yake, na kubadilisha mambo haya, na kuondoa macho yetu kutoka kwenye mambo kama hayo, na mawazo yetu, kwa mambo ya bure ya ulimwengu, kutosheleza tamaa inayoishi kwa roho ambaye tumemwacha ayatawale maisha yetu. Jinsi tunavyopaswa kuondolea mbali roho huyo, na kumpokea Roho wa Mungu!

97 Maumbile yote, kila mahali, yanashuhudia! Mbingu, anga, mambo mengi sana! Mimi, nikiketi kwenye chumba changu cha kusomea, jana, niliandika; sitapata wakati wa kuliendea. Bali unaweza tu kuangalia kote kwenye kitu chochote ambacho Mungu aliumba, kinatoa ushuhuda kwa utukufu Wake. Chochote, kiumbe chochote cha Mungu, kinatoa ushuhuda kwa Mungu, na kwa kusudi Lake. Inaonyesha Akili ya juu sana!

98 Nimesimama juu ya milima na kuangalia miti mbilikimo, mikubwa tu *hivi*, inayoliwa na kondoo, kondoo mwitu, na kuona miti hiyo ya mbilikimo *hapa* juu. Ukishuka mbele kidogo, ndipo unafikia mmeasumu, maumbile tofauti, aina tofauti inayoishi mahali tofauti. Chini kidogo, ndipo unafikia msonobari. Chini kidogo, unaingia kwenye kunde mtetemo. Kutoka kwa hiyo, unaingia kwenye kituka, kichaka. Ukishuka chini, kwenye hiyo, unaingia kwenye nyasi. Na ukishuka chini kwenye hiyo, unaingia kwenye magugu. Na ukiendelea kushuka unaingia jangwani, ambapo hakuna kitu. Kila moja, ina chembechembe na uhai wake yenyewe, tukinena juu ya mazingira yake na mahali inapoishi, ni Mungu tu mwenye akili anayeweza kufanya jambo kama hilo! Kila moja ya hiyo, ina maisha ya kibinafsi. Angalia mnazi huko Florida, angalia mwaloni katika—katika Marekani ya kati, na kunde mtetemo kwenye milima ya Rockies; kila mmoja, una maisha tofauti, ukitoa ushuhuda kwa ajili ya utukufu wa Mungu Mwenyezi.

99 Angalia bahari kuu unaposimama karibu nayo. Na mawimbi yake makubwa yenye hasira yakivunja ukingo, kwa hasira kubwa sana, hata yanavuja kwa kishindo na kuruka kama mbwa mwenye hasira aliyefungiwa mwishoni mwa mnyororo. Yangeweza kuuzamisha ulimwengu kama yangaliweza; yangechoshwa na dhambi yake. Lakini Mungu aliweka mlinzi huko juu angani, anayeitwa mwezi, kisha akaweka mipaka ya bahari, kusudi yasiweze kupita tena. Basi mlinzi huyo huiangalia, mchana na usiku. Anapogeuza mgongo wake, kumwangalia Mungu, aione sura ya Mungu, haya hapa maji yanajaa; lakini wakati anapogeuza uso wake tena, maji yanakupwa. Yeye analinda mipaka hiyo, wala hawezi kuondoka. Anapougeuza mgongo wake, maji yanajaa; lakini akiugeuza uso wake tena, maji yanakupwa upesi. Mungu ameweka mlinzi. Inafanya nini? Inatoa ushuhuda ya kwamba Mungu wa Mwanzo,

Mungu wa Biblia, angali ni Mungu! Ni ushuhuda, ya kwamba, Yeye yuko!

100 Tungeweza kuwaita wengine zaidi, wa manabii wa Agano la Kale, jinsi walivyotoa ushuhuda wa kuzaliwa kwa Kristo. Kwa mfano, katika Isaya, mlango wa 9, Isaya 9:6. Mamia na mamia ya miaka kabla halijatukia, manabii walitoa ushuhuda. Nao wakasema, "Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume." Walijuaje? Mtu aliyezaliwa na mwanamke, angejuaje jambo kama hilo? Mtu angewezaje, mamia ya miaka kabla halijatukia, kujua yale hasa yangetukia, "Kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume"? Kasema, "Ataitwa jina Lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa milele."

101 Kasema mahali atakapozaliwa. Huyo nabii, chini ya uvuvio, alisema, "Nawe Bethlehemu katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe katika majumbe wote? Bali kwako atatoka Mtawala!"

102 Ni kitu gani kilichowagusa hao manabii? Ni kitu gani kilichowavuvia? Huo usahihi mkamilifu! Si huo tu, bali hao manabii walisema atakayofanya. Manabii hata walimwona Yeye akizaliwa, mahali ambapo Yeye, angezaliwa, jinsi ambavyo angezaliwa. Si mtoto mchanga wa kawaida, mtoto tu aliyezaliwa na mwanamke fulani; Hilo lilisema Yeye angezaliwa kwa njia ya kiajabu, angezaliwa na bikira, "Bikira atachukua mimba." Ni kitu gani kingeweza kumgusa mwanadamu aliye katika hali ya kufa kumfanya aone hilo, mamia ya miaka kabla halijatukia? Sahihi kikamilifu, sahihi kabisa! Nena kuhusu ushahidi wa Mwenye uhai mkuu sana, Mungu aliye hai! Si hayo tu, bali walisema mahali atakapozaliwa, na jinsi atakavyozaliwa.

103 Wakasema yale ulimwengu ungesema juu Yake. Wakatabiri ishara zile zile hasa na mambo ambayo yangemfuata, kuthibitisha alikuwa ni Masihi. Wakathibitisha ya kwamba atakataliwa. Na hata, katika Roho, akatoa Maneno Yake msalabani akiugua, mamia ya miaka kabla hajazaliwa.

104 Daudi, katika Roho. Kama ninavyopenda kurejea kwenye jambo hilo, kama Yesu alivyosema pale, "Kwa nini Daudi, katika Roho, anamwita 'Bwana'?" Daudi, si Daudi, bali Daudi katika Roho! Ipo tofauti kubwa kati ya Daudi, na Daudi katika Roho. Kuna tofauti kubwa sana kati ya kanisa, na kanisa katika Roho. "Ni kwa nini Daudi, katika Roho, alimwita Yeye 'Bwana,' kama Yeye alikuwa ni Mwanaye, akisema, 'Bwana alimwambia Bwana wangu, "Keti mkono wangu wa kuume"'?" "Wao wangeweza kuuliza, wasingeweza kumjibu tena, kumuuliza maswali zaidi baada ya hapo."

105 Lakini Daudi, katika Zaburi ya 22, aliingia katika Roho, Roho! Na, alipoingia, hata alitoa Maneno ambayo Yeye aliyanena akiugua msalabani. "Mungu Wangu, Mungu Wangu,

mbona umeniacha? Mifupa Yangu yote, inanikazia macho! Na jinsi walivyoichoma mikono Yangu na miguu Yangu!"

106 Hata hivyo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu," yalitoka kwa yule nabii mwingine, "akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa mapigo Yake sisi tuliponywa."

107 Ule usahihi, ule ukamilifu wa manabii hao, hakuna hata Neno moja walilonena kumhusu Yeye ila lile lililotimia. Zile nabii za mwisho saba zilizotolewa juu Yake, zilijibiwa katika saa saba za mwisho pale msalabani. Jinsi ambavyo kila Neno lilitimizwa, hakuna hata kitu kimoja kilichoachwa bila kutimizwa!

108 Hilo linanena juu ya nini? Mwenye Akili nyingi sana. Haikuwa ni hao watu. Hao watu walikuwa tu ni watu kama mimi na wewe. Bali walivuviwa na Mwenye Uhai mkuu ambaye alikuwa akitoa ushuhuda ya kwamba sisi, katika kizazi hiki, na katika vizazi vijavyo, na vizazi vyote kati yao na hapa, tungeweza kuangalia Neno Lake na kujua ya kwamba ni ya kweli. Ni ushuhuda ya kwamba Neno la Mungu ni Kweli.

109 Kazi Zake zote ni kamilifu. Ni kamilifu na hazichelewi. Hazikosei saa moja. Wakati mwingine tunafikiri zitakosea, bali hazikosei. Baada ya kutimia, tunaona halingeliweza kutukia mapema zaidi, halingeweza kuwa bora zaidi. Ni kamilifu, na kwenye wakati.

110 Hata katika siku yetu leo hii, tunapoona maono haya yakitukia, na mambo yanayotukia. Nayo yanatabiriwa, na tunashangaa yatatimia lini, kile kitakachotukia. Lakini tunapata ya kwamba ni makamilifu, na kwenye wakati, hasa.

111 Ningewezaje kuwazia juu ya mama yangu, jinsi ambavyo nilimwona, mzee na akitetemeka. Lakini basi wakati aliponipa lile ono, na nikaona hali aliyomo sasa, ninamtukuza Mungu! Ninajua ya kwamba ataishi tena. Hajafa; analala. Yuko katika Kristo.

112 Jinsi tunavyoona ya kwamba Mungu amenena mambo haya kimbele! Mara ya mwisho nilipokuwa kwenye mimbara yenu, ama mimbara hii hapa, nilisimulia ono Bwana alilonipa juu ya kwenda huko Kaskazini, na yale ambayo yangetukia. Na jinsi ambavyo jamaa hao, wakishuka mlimani, wakisema, "Ndugu Branham, unataka kuniambia, mahali fulani kati ya hapa na mahali pale, nusu maili, ya kwamba kutakuwako na dubu wa kijivu, na wa fedha? Hatujapata kumwona mmoja hapo kabla! Bali utampata kabla hujafika pale."

Nikasema, "Hiyo ni kulingana na Neno Lake."

113 Na jambo hilo lilitukia vivyo hivyo tu! Kwa nini? Linatoa ushuhuda ya kwamba Yeye angali ni Mungu, ya kwamba ahadi Zake zote ni kweli. Mungu hushuhudia, na, shuhuda Zake ni

kweli. Anatoa ushahidi, na ushuhuda unamshuhudia shahidi Wake. Unanena juu ya Mwenye Akili fulani. Naam.

114 Wakati Yesu wa Nazareti alipokuja duniani, kazi Zake zote kuu zilishuhudia madai Yake. Hakuna mtu aliyepaswa (kamwe) kumtilia shaka. Yeye alisema, "Kama hamniamini Mimi, aminini hizo kazi; kama hamwezi kuona kwamba Yeye ni Mungu."

115 "Unajifanya Mwenyewe! Ukiwa mwanadamu, Wewe unajifanya kuwa Mungu."

116 Akasema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, basi aminini kazi; kwa kuwa hizo ni shuhuda za Mungu, zikishuhudia ya kwamba Mimi ni kile nilichosema nilikuwa. Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini ishara ambazo zilikuwa zinifuate Mimi. Hivi Masihi hakupaswa kufanya mambo haya?" Yeye alikuwa ni Nini? Ushuhuda! Zilishuhudia kila dai alilotoa.

117 Martha alisimama pale karibu na Yesu, huku ndugu yake akiwa amekufa na yumo kaburini. Uharibifu ulikuwa umeingia, mwili wake ulikuwa umekwisha, naye alikuwa tu anaozea mle kaburini. Wadudu walikuwa tayari wanatambaa kuingia mwilini mwake, mabuu ya ngozi. Na uso wake ulikuwa umebonyea. Lakini yeye alisema, "Bwana, tunaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni. Tuna hakika ya jambo hilo."

118 Akasema, "Mimi Ndimi ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Yeye aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe. Je! unaamini hili?"

119 Akasema, "Naam, Bwana! Naam, Bwana, ninaamini ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa aje ulimwenguni."

120 "Sasa nitakuonyesha ya kwamba Mimi Ndimi Niliyekuwa, niliyesema kwamba nilikuwa. Nitashuhudia hilo. Nitathibitisha madai Yangu, ya kwamba Mimi Ndimi ambaye Nipo. Mmemzika wapi?"

Ndipo akasema, "Bwana, njoo, uone."

121 Ndipo, akionyesha sehemu Zake za kibinadamu. Alilia pamoja na hao waliao. Anacheka na hao wachekao. Yeye yuko katika ushindi pamoja na wale walio katika ushindi. Hebu tumdumishe katika ushindi.

122 Akaenda kaburini, na akasimama pale wakati walipovingirisha na kuliondoa lile jiwe. Na pale maskini ule mwili umelazwa mle, wenye mabuu, umeoza, umelazwa ardhini, uso umebonyea, huku uharibifu ukiingia. Akasema Maneno hayo, "Lazaro, njoo huku!" Ndipo mtu huyo, aliyekuwa amekufa, akasimama kwa miguu yake na akaishi tena.

123 Hilo lilitimiza kila dai alilopata kudai, ya kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alikuwa ni zaidi ya Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa Mwana na Mungu pia. Alikuwa ni maskani ya

Mungu, maana hakuna mtu wa pili angeweza kamwe kuwa na mamlaka kama hayo. Ilihitaji Mungu Mwenyewe kuita na kurudisha uhai wa mtu ambaye amekufa na kuzikwa kwa muda wa siku nne. Kazi Zake Mwenyewe zilishuhudia kila dai alilofanya. Yeye alikuwa ni Mungu.

124 Tunajua hiyo ni kweli, maana Yeye alisema ilikuwa hivyo. Ushuhuda wa manabii. Ushuhuda wa maumbile. Ushahidi wa maumbile. Ushahidi wa manabii. Ushahidi wa Yesu.

125 Na kamwe hakujiacha bila shahidi. Mungu daima amekuwa na shahidi Wake. Na wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Yafaa Mimi niondoke; kwa maana, nisipoondoka, siwezi kumtuma Shahidi huyu; huyu Shahidi wa Milele, asiyepatikana na mauti."

126 Yeye alizaliwa na mwanamke, kwa hiyo ilibidi aharibike . . . ilibidi Yeye afe, hasa. Mungu asingeruhusu mwili Wake kuona uharibifu. Lakini ilibidi afe kama mwanadamu, ili kuziondoa dhambi zetu.

127 Lakini kabla hajaondoka, Yeye alituachia Shahidi, Roho Mtakatifu. Manabii karibu wote, kotekote katika wakati, huko nyuma kabisa katika siku za mwanzoni, walinena juu ya Shahidi huyu mkuu ambaye angekuwako katika siku za mwisho, kwa kanisa; Shahidi wetu mkuu, Roho Mtakatifu.

128 Roho Mtakatifu ndiye Shahidi wetu. Ndiye thibitisho. Ndiye muhuri. Ndiye haki zetu kamili. Ndiye hatimiliki hakiki ya kila Neno alilonena Mungu. Amina! Yeye ni shahidi ya kwamba Kristo yu hai. Na kwa kuwa Yeye yu hai, sisi nasi tu hai. Yeye ni taarifa halisi.

129 Kukiweko na Mtu kama huyo atakayekuja katika siku za mwisho, kuliongoza Kanisa, ilimpasa Mungu kuwaambia watu Wake ya kwamba Yeye atakuwa hapa. Manabii wote, karibu wote, wanashuhudia kuja Kwake, kwa Roho Mtakatifu.

130 Karne nane kabla jambo hilo halijatukia, Yoeli, mwana wa Pethueli, alitabiri ya kwamba Yeye angekuja. Miaka mia nane kabla halijatukia! Huyu mwana mashuhuri wa Pethueli, nabii; aliyedhaniwa kwamba ni jakamoyo, amerukwa na akili, ana wasiwasi, ana mhemko, hana akili timamu; alitabiri, Yoeli 2:28, na kusema:

> . . . *itakuwa,* katika siku za mwisho, asema Mungu, *nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri* . . .
>
> . . . *juu ya watumishi* wangu, *wanaume kwa wanawake, nitamimina roho yangu,* nao watatabiri.
>
> *Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu juu na nchi* chini, ishara, nguzo za *moto* na *moshi* na mvuke.

> *Na itakuwa ya kwamba,* kabla haijaja hiyo siku iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana, *kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la Bwana* ataponywa*;*

131 Miaka mia nane kabla ya kuja kwa Shahidi huyu mkuu, mwana wa Pethueli alishuhudia Hilo, akatabiri habari Zake. Ni kitu gani kilichomgusa maskini jamaa huyo?

132 Niambieni ni kitu gani kingeweza kumwambia mtu, ambaye "alizaliwa na mwanamke, wa siku chache zilizojawa na shida." Hivyo ndivyo alivyo. Niambieni ni kitu gani kingaliweza kuchochea utu wake wa ndani kabisa, kiasi kwamba angeweza kuangalia kupitia anga na wakati, na kumwona Shahidi huyu mkuu akija kanisani katika siku ya mwisho. Niambieni ni kitu gani kingaliweza kufanya hivyo. Hakuna kitu ila Mwenyezi Mungu, mwenye akili, mkuu sana, mwenye nguvu nyingi! Hicho ndicho kitu pekee kingaliweza kufanya jambo hilo. Kumgusa mwanadamu, "Mtu aliyezaliwa na mwanamke, na aliyejaa shida, na ni wa siku chache," kama Ayubu 14 ilivyosema. "Anatokea kama ua, anakatiliwa mbali; naam, anakwisha, anatoa roho yake." Lakini, juu ya mtu kama huyo, Roho, akili za Mungu mwenyezi na mwenye nguvu zinaweza kuvunja vizuizi vyote na wakati, zipenye mle kwa Roho Wake, na kumwonyesha mwanadamu yatakayotukia. Haleluya!

133 Kama huo si ushuhuda wa Mungu aliye hai, ni kitu gani? Ambao unaweza kutabiri jambo kabla halijatukia! Amina. Ambao unaweza kuliona kabla halijatukia! Na kulitabiri, kwa akili, na usahihi mkamilifu hata linatukia jinsi hasa yeye alivyolisema. Kama huo si ushuhuda, ni kitu gani? Ni kitu gani kingeweza kunena zaidi juu ya Mungu aliye hai? Hakika, Yeye ni shahidi!

134 Alitabiri ya kwamba ingetimia, "Katika siku za mwisho, ya kwamba Yeye angemimina Roho Wake juu ya wote wenye mwili."

135 Miaka sabini na mitano baada ya Yoeli kutabiri. Isaya, mwana wa Amozi, alitabiri juu ya Shahidi huyu mkuu aliyekuwa alijie Kanisa.

136 Ninazungumza juu ya kitu gani? Shahidi, shahidi wa kweli, shahidi halisi; tumemleta kupitia kwa maumbile, kupitia kwa manabii, kupitia kwa Biblia. Sasa tunampata, tukishuka chini hata kwenye siku ambayo atatolewa.

137 Miaka sabini na mitano, karibu miaka sabini na mitano baada ya Yoeli kutoa unabii, ndipo Isaya akasema. Mwana wa Amozi, yule nabii mkuu aliyetoa Biblia nzima, kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo, katika milango yake sitini na sita; kama kitabu, kina vitabu sitini na sita ndani yake. Naye alianzia na uumbaji, katika Mwanzo, na kumalizia katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Mtu huyu mashuhuri, alitabiri kuhusu kuja kwa Roho Mtakatifu.

138 Hebu turudi tu nyuma na kusoma. Nina Isaya 28:11. Hebu tusome tu kwa muda mfupi, na tuone hapa yale aliyosema juu ya kule kuja kwa Roho Mtakatifu. Isaya, mlango wa 28, hebu tuanzie kwenye kifungu cha 5.

> *Katika siku ile Bwana wa majeshi atakuwa ni taji ya fahari...*

139 Yeye ananena juu ya siku hii, kuu ambapo yule Shahidi angekuja. Taji yetu ni nini? Roho Mtakatifu anatuvika taji!

> *...taji ya fahari, na kilemba cha uzuri, kwa mabaki ya watu wake,*

140 *Mabaki*, wale "watu waliosalia." "Atakuwa kilemba, taji ya fahari, kilemba cha uzuri!" Wazia, hii ni miaka mia saba kabla halijatukia!

> *...atakuwa roho ya hukumu* kwake yeye *anayehukumu*...(Hilo ndilo analotufanyia madhabahuni.)

> *...naye atakuwa nguvu kwao wageuzao nyuma vita langoni.* (Hebu nione.)...*wageuzao nyuma vita*... *langoni.*

141 Hao wanaosimama kwa ajili Yake na pamoja Naye, Roho huyu mkuu (Roho Mtakatifu aliyetabiriwa) atakuwa ndiye nguvu zake anayesimama langoni, vitani. Yeye ni nguvu zetu. Tunamtegemea Yeye; si mila, si elimu, si mambo ya ulimwengu. "Si kwa nguvu, si kwa uweza, bali ni kwa Roho Yangu, asema Bwana." Kanisa linasimama kwa uchaji juu ya jambo Hilo! "Yeye atakuwa nguvu zake anayesimama langoni." Si msingi wake wa kitheolojia, si dhehebu lake, bali Roho Mtakatifu atakuwa ni nguvu zake. Atakuwa ndiye atakayesimama langoni. Atategemea nguvu za Roho Mtakatifu kumfukuza mgeni.

> *Lakini hawa nao wamekosa kwa divai,* (sasa sikilizeni)*, wamepotea kwa kileo;* wamepoteza *"ile"* njia; *kuhani na* manabii *wamekosa kwa* kileo*, wamemezwa kwa divai, wamepotea kwa kileo; hukosa katika maono,* na *hujikwaa katika hukumu.*

142 Kwa maneno mengine, katika *ono*, hata hawaamini kitu kama hicho. Na katika *hukumu*, wao wanasema, "Loo, mradi tu, unajiunga na kanisa, ni sawa." Ndipo tuna nini? Kundi la walevi. Angalia yale aliyosema nabii. Huyu hapa shahidi wa Mungu.

> *Maana meza zimejaa* uchafu*, zimejaa matapiko na uchafu, kwa hiyo hapana sehemu iliyo* safi.

143 Hakuna mahali palipo safi; zile meza. Mbona, wanaingia, walevi na malaya, na—na kuchukua kipande cha mkate mwembamba na kukikata, na kufanya ushirika, ambapo walio safi na wasio safi wanakula pamoja. Matapiko! Meza zimejaa matapiko.

> *Atamfundisha nani maarifa* katika siku kama hiyo? *Atamfahamisha*. . .*nani habari hii?*

144 Wangemfundisha nani, wakati wana matukio yao wenyewe ya kitheolojia na kadhalika wanayotegemea? Hawatarudi kwenye Neno la Mungu. Wanasema, "Loo, hilo lilikuwa ni kwa ajili ya mahali pengine. Hilo ni kwa ajili ya kizazi kingine." Meza zao zimejaa matapiko. Msikilize nabii huyu akiwa na akili hii ya hali ya juu ya Mungu akizungumza kupitia kwake.

> . . .*wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini?* (Si, watoto wachanga wa kanisa!)

> *Kwa maana ni amri juu ya amri*. . .

145 Yeye anazungumza juu ya Neno sasa. Usiseme "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," wakati Hilo lilisema "Jina La Yesu!" Usiseme "peana mikono," wakati Yeye alisema "kuzaliwa mara ya pili!"

> . . .*amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya*. . .*kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo.*

> *La, bali kwa kugugumiza maneno, na kwa* lugha nyingine *nitasema na watu hawa.* (Haleluya!)

146 Kwa midomo *ya kugugumiza maneno,* "mnong'ono." Labda kusanyiko limeketi tu, katika uchaji na ukimya, mtu fulani. . .mtu anaweza kushika mnong'ono huo na kufahamu wanayosema. "Kwa midomo ya kugugumiza maneno na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa," akitabiri juu ya Roho Mtakatifu. "Midomo ya kugugumiza, nitasema na watu hawa."

> *Ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha* . . .

147 Sasa, ninyi ndugu wa Sabato mnaochukua siku ya saba, na hii je?

> . . .*Hii ndiyo* Sabato*, Hii ndiyo raha yenu* ambapo mnaweza *kumpa raha yeye aliyechoka;*. . .

148 Mungu, tupe watu hodari watakaosimama langoni na Hilo, na kulishuhudia!

> . . .*Hii ndiyo raha yenu* ambapo mnaweza *kumpa raha yeye aliyechoka;*. . .*huku ndiko* kuburudika*;* bali *hawakutaka kusikia.*

149 Hiyo ndiyo sehemu yenye huzuni, hawangesikia Hilo. Walitikisa vichwa vyao, na kufanyia mzaha na dhihaka, na kuendelea.

150 Lakini Isaya alitabiri, na kusema ya kwamba, "Itakuwa ya kwamba Yeye atatuma Roho Wake, na itakuwa ni taji ya fahari kwa Kanisa, na nguvu kwa yeye anayesimama langoni." Tungejuaje ya kwamba ilikuwa ni Roho? Kasema, "Maana, kwa midomo yenye kugugumiza maneno na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo raha na kuburudisha."

151 Lakini, kwa Haya yote, walitaka mashirika yao na madhehebu yao. Nao wakafuatilia meza zao zenye matapiko na ulimwengu, na wakachanganyikana na anasa za mambo ya ulimwengu. Hawajazaliwa mara ya pili. Wanaziacha zile Kweli, na kuyaendea mambo ya ulimwengu; na kuifanya nyumba ya Bwana kuwa machukizo ya uchafu, ambako wana madansi na karamu, na vurugu; na wanawake wamevaa nguo mbaya na kaptura, na kukata nywele zao, na kutumia vipodozi; na vitu vyote kama hivyo, kama vile Biblia ilivyotabiri!

152 Isaya alisema ya kwamba wangefanya hivyo. Isaya, mlango wa 5 na wa 6. Isomeni, jinsi ambavyo alisema ya kwamba wanawake wangefanya hivyo katika siku za mwisho. Mashahidi wa Mungu ni wa kweli. Walitumainia upuuzi wa ulimwengu, badala ya nguvu za Mungu, kuwaokoa. Sasa, hiyo ilikuwa ni miaka sabini na mitano baada ya Yoeli.

153 Miaka thelathini baada ya kuzaliwa kwake Yesu. Nimeandika manabii wengine wengi hapa chini. Lakini miaka thelathini baada ya kuzaliwa kwake Yesu, kulikuwako na yule mtawala miongoni mwa manabii, (loo, jamani) Yohana Mbatizaji! Watu wote walijua ya kwamba alikuwa ni nabii aliyetoka kwa Mungu, mtangulizi wa kuja kwa Kristo. Ambaye amebashiriwa tena, katika siku za mwisho!

154 Yesu alisema, "Mlitoka mkaenda kuona nini, unyasi unaotikiswa na upepo wowote, dhehebu lolote linampindua *huku* ama *kule*? Si Yohana!" Kasema, "Mlitoka mkaenda kuona nini, mheshimiwa akiwa na namna fulani ya tabibu wa akili, kuweka nguo zake *hivi-na-hivi*, na kumwambia jinsi anavyopaswa kuvalia?" Ndipo akasema, "Watu wa namna hiyo huwabusu watoto wachanga na wanaishi katika majumba ya wafalme, na wanazungumzia shule za umma, na kadhalika; yeye si askari wa vita, hayuko kwenye mstari wa mbele wa vita, hajui jinsi ya kutumia Upanga ukatao kuwili. Mnaona, hao ndio wanaofanya hivyo. Lakini mlitoka kwenda kuona nini, nabii?" Akasema, "Sasa, ninasema, zaidi ya nabii!"

155 Msikilize mtawala huyu mashuhuri, akija amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo, akiishi kwa mimea ya mwituni. Haleluya! Hana tukio la theolojia ya seminari nyuma yake; bali tukio la kwamba alikuwa amenena na Mungu, naye alizaliwa kwa kusudi la kufanya hivyo. Neno lilisema ya kwamba atakuja. Naam, bwana. Akatoka akatembea ukingoni mwa Yordani, miguu yake ikiwa matopeni, kasema, "Msifikiri, enyi Mafarisayo mnaosema 'tuna Ibrahimu Baba yetu,' kwa maana nawaambia, Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

156 Huyo mtawala wa manabii, yule aliyekuwa na majaliwa ya kumtambulisha Masihi na aliyeona ishara ya Masihi na akaitambua, wakati ile Nuru iliposhuka kutoka Mbinguni

ikakaa juu Yake, alikuwa ni shahidi wa jambo hilo! Yeye alisema nini juu yake? Haya hapa maneno yake, aliyosema yule nabii kama shahidi.

> *Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye* ajaye *nyuma yangu, ambaye ana nguvu kuliko mimi, viatu vyake sistahili hata kuvifungua; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu, na kwa moto.*
>
> *Na pepeto* lake *li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake; na kuikusanya ngano yake ghalani,* bali. . .atateketeza *makapi kwa moto usiozimika.*

157 Yeye alitabiri ya kwamba Shahidi wa Kanisa angekuja, Roho Mtakatifu! "Kweli mimi ninawabatiza kwa maji; hiyo ndiyo huduma yangu. Nitawabatiza kwa maji, kwa ajili ya toba." Haleluya! "Lakini kuna Mmoja ajaye nyuma yangu! Ninashuhudia jambo hili kwa maji, bali kuna Mmoja ajaye ambaye atatuma kitu kikubwa zaidi. Atamtuma Shahidi mwingine; si maji, bali ni Roho! Atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto." Haleluya! Shahidi wa Mungu, atawaondolea ufuasi wote wa kanisa! "Atawapa shahidi wa kweli, kwa kuwa atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto. Na pepeto Lake li mkononi Mwake. Shoka limewekwa kwenye shina la mti; na kila mti usiozaa matunda mazuri, utakatwa na kutupwa motoni. Kwa hiyo, tubuni, iweni tayari, kwa kuwa saa imekaribia." Mtawala huyo mkuu, jinsi alivyokuwa ni nabii mkuu!

158 Miaka mitatu baadaye, akiisha kutabiri, Yesu Bwana wetu alikuwa amemaliza huduma Yake, huduma Yake ya duniani. Kasema, "Yafaa kwenu kwamba Mimi niondoke. Kwa maana, nisipoenda Zangu, Roho Mtakatifu hatakuja. Lakini Mimi nitamtuma. Kitambo kidogo. . .Nanyi mnataka kujua Yeye ni nani. Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari."

159 Katika Luka 24:49, mwishoni mwa huduma Yake, wakati huduma yake ya duniani ilipomalizika, Yeye alisema, katika Luka 24:49, "Tazama, nawaletea ahadi ambayo shuhuda hizi zimesema. Nawaletea ahadi ambayo Isaya alinena habari zake. Nawaletea ahadi ambayo Yoeli alisema habari zake. Nawaletea ahadi ambayo manabii wote, ambayo Baba alionyesha kupitia kwa manabii, nawaletea ahadi ya Baba Yangu juu yenu."

> *. . .tazama, nawaletea ahadi ya Baba yangu juu yenu: lakini* ngojeni *hapa mjini Yerusalemu*. . .Acheni mahubiri yenu, acheni kuimba, msifanye lolote bali nendeni kule mjini *Yerusalemu,* na mngoje *hata mvikwe uwezo utokao juu.*

160 Ulikuwa uwe shahidi wa namna gani? Ati "Ngojeni Yerusalemu hata mtakapokamilisha miaka ishirini ya shule ya

upili ama seminari"? "Ngojeni mpaka mtakapopokea Digrii ya kwanza ya Sanaa"? "Ngojeni hata mtakapojifunza ku—kunena katika lugha zingine, ili kwamba, ikitokea kwamba awaite hudumani, mngeweza kuzungumza katika hizo"? La, haikuwa hivyo.

161 Hebu tu Nguvu zitokazo Juu zije, zitajishughulikia zitakapokuja. "Ninyi ngonjeni hata mvikwe Uwezo." Ee Mungu, mbona watu hawawezi kuona hilo? Si kujiunga na kanisa. Ni kungojea Nguvu! "Ngojeni hata mvikwe, Nguvu zitokazo Juu, kwa maana nitamtuma. Yeye ni ahadi ya Mungu, Nami nitamtuma. Nitashuhudia! Yeye, atakapokuja, atashuhudia! Kwa kuwa, hatanena habari Zake Mwenyewe, bali atanena habari Zangu Mimi." Amina.

162 Angalieni kile atakachofanya. "Atawakumbusha mambo haya niliyowafundisha." Si kitu fulani cha seminari. Ati nini? "Ataleta mambo haya niliyowafundisha, awakumbushe, ya kwamba ni Maneno ya Mungu. Mtasahau yote kuhusu ujuzi wenu wa seminari. Mtayapata mambo *haya*, Maneno ambayo nimewafundisha. Atawakumbusha mambo hayo. Na, Yeye atafanya jambo lingine, atawaonyesha mambo yajayo." Huyo ni Shahidi wa kweli. Huyo ni Shahidi wa kweli wa Mungu. "Atawarudishia Injili, huyu Roho Mtakatifu! Ingawa huenda akaachwa kwa karibu miaka elfu mbili, huenda wataikanyaga chini ya miguu yao, kwenye theolojia ya kujibunia; bali Yeye ajapo, atawarudisha Kwake. Si hivyo tu, bali atawaambia mambo yajayo. Atanena kupitia kwenu, kwa midomo ya kugugumiza maneno na kwa lugha zingine. Atafanya mambo haya yote. Kila kitu ambacho Mungu ameahidi, Yeye atafanya. Nina . . . Nitawaletea ahadi ya Baba."

163 Huko Pentekoste, wakati Huyo alipokuja, wao walisema nini? Walisema, "Sisi ni mashahidi Wake. Sisi ni mashahidi ya kwamba mambo haya ambayo yamesemwa yametimia." Loo, jamani! Hilo linanifanya kujisikia wa kidini. Walipokuwa wamesimama pale, walisema, "Sisi ni mashahidi Wake. Hatuna digrii." Walikuwa ni nini? Waongofu, baadhi yao walikuwa ni Wayahudi, wenye sifa, waliokauka na wagumu, yote yalikuwa yameondolewa kwao!

164 Angalia Simoni Petro aliyejiendeleza mwenyewe, jinsi alivyofikiri ya kwamba alikuwa ni mgumu sana. Asingekula chochote kichafu.

165 Vipi kuhusu Paulo aliyejiendeleza mwenyewe, akiyatesa makanisa kutoka kila mahali! Ilikuwaje wakati alipokutana na Huyo, yule Roho Mtakatifu, akienda zake Dameski siku ile? Alisimama mbele ya Festo na kusema, "Mimi si mwendawazimu. Bali kwa njia ile ambayo waiita uzushi, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu."

166 Wao walisema, "Sisi ni—sisi ni mashahidi Wake." Sasa, kulikuwako na mashahidi watatu dhahiri huko Pentekoste.

167 Kwanza, Neno la hao manabii, ya kwamba Mungu angeimwaga Roho Yake katika siku za mwisho juu ya watu. Ushahidi ambao manabii walikuwa nao, uliokuwa ni Neno la Mungu, ulikuwa umetimizwa! Huo ulikuwa ni ushuhuda mmoja, ujumbe wa manabii ulitimizwa! "Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Watakuwa na midomo inayogugumiza maneno, na kwa lugha zingine nitanena na watu hawa." Hiyo hapo. Wasingeweza kuikana. Halafu, kulikuwako na mashahidi watatu. Huyo alikuwa ni mmoja, ya kwamba Neno la manabii lilikuwa limetimizwa.

168 Shahidi mwingine, alikuwa ni watu. Walikuwa wakishuhudia, "Jambo fulani limetukia!"

169 "Nilikuwa nimejificha mle juu chumbani. Nilikuwa mwenye soni sana. Niliona aibu. Na—na—najua alikuwa ameondolewa, na ni—niliona aibu mbele ya kundi hili la kiungwana hapa. Niliwaonea aibu. Niliona aibu ya kwamba mimi, labda, sikutaka kusema lolote juu yake, kwa sababu nilihofu ningeanzisha jambo fulani la mhemko, ama chochote kile."

170 Hiyo ndiyo shida ya makanisa haya ya kujitengenezea siku hizi. Yanahofu watasababisha usumbufu mwingi sana. Wanahofu watafanya jambo fulani lisilo sahihi. Loo, enyi, wa kujiendeleza, wenye kujiridhisha! Tunachohitaji ni pentekoste! Tunachohitaji ni kujazwa, kuja kwa Roho Mtakatifu!

171 Wao walisema, "Sisi ni mashahidi Wake, kwa sababu tumejazwa Naye!" Petro alisema, "Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili. Watu hawa hawajalewa kama mnavyodhania, kwa maana ni saa tatu ya mchana. Lakini jambo hili ni Lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.' Tunashuhudia ya kwamba Maneno ya manabii ni ya kweli, kwa maana tumejazwa sasa!" Loo, jamani!

172 Hiyo ndiyo tunayohitaji. Hiyo ndiyo kanisa linahitaji. Hiyo ndiyo hawa, watu milioni mia moja na sabini wanaokiri kuwa Wakristo kote ulimwenguni, wanayohitaji, ni pentekoste nyingine! Si kurudi na kusoma miaka ishirini na mitano; bali kujazwa na Roho Mtakatifu, shahidi ndani yako, akishuhudia juu ya ufufuo wa Kristo, na kwa Neno la Mungu. "Yohana aliketi kwenye kisiwa cha Patimo, kwa ajili ya Neno la Mungu, ushuhuda wa Neno la Mungu."

173 Hapo Neno la manabii lilitimizwa. Hapo palikuwapo na watu walioshuhudia. Na hapo alikuwapo Roho Mtakatifu Mwenyewe! Hao hapo watatu. Nayo Biblia ilisema, "Katika kinywa cha mashahidi watatu, kila Neno na lihakikishwe." Hiyo ni kweli.

Hapo Neno la manabii lilitimizwa.

174 Hapo palikuwapo watu, waliosema, “Jambo fulani limetukia kwangu! Jambo fulani limetukia! Mimi siogopi tena. Siogopi mauti. Siogopi kitu. Jambo fulani lilitukia! Nilisahau theolojia yangu yote. Nilisahau mapokeo yangu yote ya kujibunia. Jambo fulani limetukia! Lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu, watu hawa hawajalewa!” Wao, walipoteza hadhi yao yote. Walilewa tu kwa Roho! Ninii tu . . .

175 Hilo ndilo tunalohitaji. Hilo ndilo tunalohitaji, kundi la watu wenye busara, wenye akili timamu wanaoweza kuinuka na kumwendea Mungu, na kusema, “Bwana, usinifanye mfuasi wa kanisa, bali nifanye shahidi! Nimwagie Roho Wako, na unijaze. Jalia niwe shahidi Wako.” Hilo ndilo tunalohitaji. Hilo ndilo kanisa limepungukiwa nalo siku hizi. Hali yake ya kupungukiwa na damu, ni kwa sababu limeikataa Damu ya Yesu Kristo.

176 Naam, Roho Mtakatifu anashuhudia, Mwenyewe, akisema, “Ndivyo ilivyo!” Hao hapo. Na watu hao wasingeweza kulikanusha.

177 Watu hawa hawakuwa wamengojea shuleni kupata elimu yoyote kubwa. Walikuwa ni watu wasio na maarifa na wasio na elimu, wavuvi na wakulima wadogo. Walikuwa ni watu wa kawaida. Biblia ilisema, “Watu wa kawaida walimsikia Yesu, kwa furaha.” Si makabwela, la, si waheshimiwa, bali, “Watu wa kawaida walimsikia, kwa furaha.” Na hapo walikuwapo watu wa kawaida, walikuwa wamemsikia, nao wakasema, “Sisi ni mashahidi ya kwamba tumepokea kitu Fulani; nasi hatujui, karibu hatujui, lugha yetu wenyewe.”

178 Bali hao watu wakasema, “Tunawaelewaje? Hawa wote si Wagalilaya?” Wagalilaya walikuwa tabaka duni la watu. Kasema, “Tunawasikiaje hawa Wagalilaya wakisema katika lugha yetu wenyewe tuliyozaliwa nayo?”

179 Wakitoa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, wakishuhudia ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa limetimizwa! “Nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili. Na kwa midomo inayogugumiza maneno na kwa lugha zingine nitasema na watu hawa, na hii ndiyo raha.” Wakishuhudia; shahidi. Huu ndio ushuhuda wake. Hakika.

Walikuwa na mashahidi watatu. Ati nini?

180 Neno la manabii, Neno la Mungu. Kwa sababu, manabii hao hawakusema neno lao, bali lilikuwa ni Neno la Mungu kama alivyoliweka kinywani mwao.

181 Nimeketi hapa sasa nikimwangalia maskini Mnorwe mmoja, tabibu, daktari, daktari wa tiba anayeketi hapa, aliyekuja kutoka mbali huko Norway, amekuja hapa kuombewa. Na hivi majuzi usiku, tulipokuwa tumeketi pamoja katika mahojiano ya faraghani, Roho Mtakatifu aliingia chumbani.

182 Akasema, “Ninangojea, Ndugu Branham, kuona kile kitakachosemwa.”

183 Hapo Roho Mtakatifu akashuka akapitia kwenye maisha yake, huko nyuma kabisa mpaka ambapo jambo fulani lilitukia, kamwambia habari zake na kilichotukia, na ni hali gani, yote kuhusu hilo, na kumwambia jambo hilo. Ilikuwa ni kitu gani? Roho wa Mungu akitoa ushuhuda!

184 Labda kuna maskini jamaa mwingine anayeketi hapa, pia, aliyetumwa na kanisa la Ndugu Palmer. Amechanganyikiwa kabisa, wala hajui la kufanya, naye alisumbuliwa sana na jambo fulani. Maskini jamaa mzuri; nafikiri alienda nyumbani. Lakini kulikuwako. . .alimtuma hapa. Ndugu Palmer aliniandikia barua, na kusema, “Ndugu Branham, ninajua ni wakati wa shughuli nyingi,” ama kitu kama hicho, “lakini wakati unapoweza kupata nafasi, mwone, kwa maana ni ndugu mzuri.” Na—na kanisa lilikuwa limemtuma huku. Alikuwa kwenye mahojiano. Wakati akiketi pale, kitu hiki kilichokuwa ndani kabisa ya moyo wake, kabla hajapata nafasi ya kusema lolote, Roho Mtakatifu aliingia ndani akakipata, akakitoa, akamwonyesha. Naye akashangilia, na machozi yakatiririka mashavuni mwake. Kwa nini? Mungu akishuhudia! Kwa njia gani, kwa William Branham? La, bwana. Kwa Roho Mtakatifu! Amina. Huyo ndiye Shahidi wa Mungu.

185 Hebu niwaambieni jambo lingine. Kwa nini. . .Maskini jamaa huyu anayeketi hapa, anayeitwa Higginbotham, shemasi aliyekuwa hapa kanisani; alitumikia wakati wake, na sasa ni mshiriki tu mwaminifu. Aliinuka, asubuhi ya leo, kunena kwa lugha, ninaamini, na kutabiri. Kwa nini Roho huyo Mtakatifu, alisema, asubuhi ya leo, wakati alipokuwa anatoa fasiri yake, “Nimemtia mafuta mtumishi wangu kuwaletea mambo ambayo mnapaswa kujua”? Loo, loo, loo! Kwa nini? Nami nilimsikia nikisimama hapa, nikiwa nimeinamisha kichwa changu, nilikuwa ninaficha machozi moyoni mwangu. Mtu huyo hakujua zaidi, sikuwa nimemwambia lolote ama mtu yeyote yule, yale nitakayohubiri, maana ndiyo kwanza nije mimbarani. Naye huyo hapo, akafunua somo, na kuwaambia watu wajiweke tayari kwa ajili Yake. “Nitasema nanyi,” kasema, “nimemtuma katika mataifa mengi, kwa watu wengi, Ujumbe uu huu. Nami nitasema nanyi, asubuhi ya leo. Utilieni maanani,” akasema, “kwa kuwa nimemtia mafuta na kumtuma huku.” Ee Mungu! Ni kitu gani? Roho Mtakatifu, Shahidi wa kweli wa Mungu. Ni kitu gani? Uungu ukifanywa mwili katika mwanadamu! Haleluya!

186 Ati nini? Kanisa, hiyo ndiyo sababu siwezi kuchukua ubatizo wa Roho Mtakatifu wa kulia, kutetemeka, ama kunena kwa lugha, au mhemko wowote. Yote ni sawa, sasa. Mnaona? Hayo, mambo hayo ni sawa, lakini ibilisi anaweza kuiga hayo vizuri sana.

187 Lakini Roho Mtakatifu ni Uungu, Mungu aliyefanyika mwili katika mwanadamu! Ni zaidi ya mhemko. Ni zaidi ya kunena kwa lugha. Ni zaidi ya kupaza sauti katika Roho. Ni zaidi ya kulia. Ni zaidi ya kujiunga na kanisa. Ni Mungu akiishi ndani ya mwanadamu. Uungu, Mungu Mwenyewe akifanyika mwili katika mtu huyo, ambapo anaweza kunena na ni kama tu Mungu Mwenyewe akinena, hilo ndilo Kanisa la Yesu Kristo. Hivyo ndivyo lile Kanisa la kwanza la kimitume lilivyoenenda.

188 Ni tofauti jinsi gani, makanisa ya siku hizi! Ni tofauti jinsi gani, kwamba tumeenda mbali Naye, tangu shirika letu la kimadhehebu lilipoanza, yapata karne ya pili baada ya Kristo, katika kanisa Katoliki la mwanzoni, lilipounda madhehebu, na kufundisha filosofia ya mwanadamu.

189 Leo hii, kuna watu wengi, sisi ni watu watenda-mema. Tunajiunga na kanisa. Nisikilizeni. Haya hapa ndiyo Ndugu Higginbotham aliyokuwa akizungumzia asubuhi ya leo; si Higginbotham, bali Roho Mtakatifu alinena kupitia kwake. Sisi ni watu watenda-mema. Tunajiunga na kanisa, nasi tunataka kuwa watu wanaopendana sana na wazuri sana. Mnaona? Hatutaki kabisa kumwudhi mtu yeyote, hakika hatutaki. Tunataka—kuwa Mkristo mzuri sana. Tunataka tunataka kujiundia Kristo.

190 Kristo haundwi! Haleluya! Loo, laiti ningalipata Maneno ambayo Mungu angenipa, kusudi mpate kuona ninalomaanisha.

191 Kondoo haombwi kutengeneza sufu. Haombwi kutengeneza sufu mwaka huu. Kama yeye ni kondoo, atakuwa na sufu kwa maana yeye ni kondoo. Haimbidi kusema, "Vema, sasa mi—mimi—mimi. . .Ninaamini mimi ni kondoo, kwa hiyo afadhali nifanye bidii hapa, sina budi kumtolea bwana wangu sufu." Haimpasi kujisumbua na hilo. Mradi yeye ni kondoo, atatoa sufu. Haimbidi kujitengenezea.

192 Sasa, haikubidi kujitengenezea uchaji wa kujibunia, na, "Mimi, yanibidi. . .mimi, sasa sipaswi kufanya jambo *hili*, ninajua mimi ni Mkristo." Loo, ndugu, kujaribu kujiokoa mwenyewe kwa nafsi yake, kwa jitihada zake za kibinadamu! Hata hivyo, ni mwaminifu.

193 Shida yake, ni mimbara hafifu, shule hafifu, seminari hafifu. Hiyo ndiyo shida yake, kufundisha theolojia za kibinadamu! Wanatoa. . .Unasema, leo, nguvu za Mkristo, wao wananinii tu. . .

"Je! wewe ni Mkristo?"

"Loo, mimi ni Mmethodisti."

"Wewe ni Mkristo?"

"Loo, mi—mi—mimi ni Mbaptisti."

Sasa, hizo ndizo nguvu za Ukristo.

194 Ni tofauti jinsi gani! Haleluya! Ni tofauti jinsi gani na Kanisa lile la mwanzoni! Hawakuwa na mambo haya ya kusema. Bali walikuwa wamejazwa na Uweza fulani, Nguvu za Roho Mtakatifu, ambazo zilikuwa zimewaweka huru na dhambi na mauti. Hawakuwa ni wa jina tu. Walikuwa na upendo wa Mungu ukiwaka mioyoni mwao, uliowapeleka mautini.

195 Becky, binti yangu, alikuwa akinisomea, *Wapiganaji wa Maonyesho*, hivi majuzi usiku. Kasema, "Sikiliza hii, baba." Na siwezi kwa wakati huu, nasikitika, siwezi kukumbuka jina hilo. Bali ki—kijana Mkristo alikuwa ametupwa nje, kama mpiganaji wa maonyesho, apate kupigana kwenye uwanja wa michezo wa Rumi.

Nimesimama katika uwanja huo wa michezo, nikiomba. Zile kuta za kale zinaporomoka.

196 Na wakati wangeketi pale, na wao—wao walipenda tu kuwaona. Iliwabidi kuuana. Mungu akinena. . . Katika siku za kale, wa—walikutana tu na kuuana, na ni hayo tu. Mungu hakupendezwa na hilo.

197 Na mmoja wa hao. . . moja ya—ya dalili za kwanza kabisa za Ukristo, alikataa kumuua mtu. Hiyo ni kweli. Nawe unaweza kumuua kwa njia nyingi zaidi kuliko kumchoma tu na kisu; msengenye, kuna njia nyingi unazoweza kufanya hivyo.

198 Lakini huyu mpiganaji wa maonyesho, walimfungulia simba. Na kwa nguvu na uweza wa Mungu, alimuua huyo simba kwa upanga wake, kisu. Watu wakapiga makofi; ulikuwa ni ushujaa. Wakasimama. Wakamfungulia mwingine, naye akamuua kwa upanga wake. Ndipo basi wakamfungulia mtu, kafiri Mwafrika mweusi, mnene, mkubwa mno, mrefu. Basi ilimbidi Mkristo huyu apigane naye, jambo ambalo yeye hakutaka kufanya. Lakini, katika hayo mapigano, alimbwaga yu—yule Mwafrika chini, kisha akaweka upanga wake papo hapo juu yake. Hakika, yule Mwafrika alisema, "Bwana, niue upesi, kusudi nisiteseke. Usinitese. Niue upesi!"

199 Huyo Mkristo akautupa upanga wake, akavua silaha zake, akaenda mbele ya mfalme mkuu, na kusema, "Mfalme mkuu, mimi ni Mkristo. Bwana na Mwokozi wangu ametukataza kuuana. Nitamwua mnyama pori, bali si ndugu yangu. Ninakataa kumuua mtu."

200 Wafalme wote wa Rumi, na kadhalika, wakasimama, na kusema, "Unataka kuniambia mtumwa mpiganaji wa maonyesho atakataa kuitii sauti ya Rumi?"

201 Ndipo wakamwita mtu huyo, "Ruka juu, ukachukue upanga ule na kumuua!" Akaruka juu, akauchukua upanga wa yule Mkristo. Yule Mkristo, bila silaha, akanyosha mikono yake. Ndipo yule mtu akamchoma moyoni mwake, kwa upanga; papo hapo kupitia moyoni mwake, kwa upanga. Na wakati mbubujiko, kati ya damu ikitoka kwa nguvu, na kuyajaza

mapafu yake, wakati kisu hiki kikubwa kilipopitia katika mapafu yake, maskini yule Mkristo akapiga magoti yake, na kusema, "Bwana Yesu, ipokee roho yangu." Na ati sisi tunanena kuhusu kuteseka kwa ajili ya Kristo? Ushuhuda wetu utakuwa nini, kukiweko na watu kama hao?

> Loo, imani ya baba zetu! ingali inaishi
> Ijapokuwa kuna gereza, moto, na upanga.

202 Hao walikuwa wanaume, ambao kumkiri Kristo kulimaanisha mauti. Walikuwa ni nini? Walikuwa wamepokea yule Shahidi. Walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu. Hao Wakristo wa kwanza hawakuogopa mauti. Baada ya hayo, Himaya ya Kirumi iliona ya kwamba kulikuwako na kitu fulani kuwahusu. Walifanya nini? Waliichagua, wakaondoka na kufanya madhehebu kutokana nayo; na kuwaingiza tu kwa kukiri, bila ya kumpokea Shahidi huyu.

203 Na hapo ndipo tulipo leo hii, Mlutheri, Mbaptisti, Mpresbiteri, na Wapentekoste wengi sana, wanavyojiita, tunashuka kwenda katika safari hii bila ya kumpokea Shahidi wa Mungu. Na Roho Mtakatifu ndiye Shahidi wetu. Naam, bwana. Ni tofauti jinsi gani, hayo makanisa ya siku hizo!

204 Kanisa la siku hizi ni, "Jiunge tu na kanisa." Kama ule msemo wa kale usemavyo, "Mtu anapojiunga na kanisa, anavaa koti jipya." Hiyo ni kweli. Lakini anapojazwa na yule Shahidi, wao wanaweka mtu mpya ndani ya koti. Si koti jipya juu ya mtu huyo; ni mtu mpya ndani ya koti! Kile tunachohitaji siku hizi ni watu wengine wengi wapya ndani ya koti! Hilo ni koti la kasisi, ninalozungumza juu yake. Naam, tunalihitaji vinginevyo. Wale wa mwanzoni . . .

205 Kanisa hili siku hizi linajaribu kujiokoa lenyewe, kwa matendo yake mema. "Loo, mimi ni Mkristo, sina budi kuwa mzuri kweli kweli. Sina budi kufanya jambo *hili*."

206 Lakini kanisa hilo la kwanza, walikuwa wakifanya nini? Wakingojea. Si kujaribu kujibadilisha, bali walikuwa wakimngojea Mungu Mwenyewe aje awabadilishe, kutoka kwa Mafarisayo, wawe mashahidi.

207 Na kile tunachohitaji leo hii ni kungojea kwingine kwa Roho Mtakatifu, yule Shahidi wa Mungu, aje atubadilishe kutoka kwenye kundi la Mafarisayo, baridi na waliokauka, atufanye mashahidi wa ufufuo wa Yesu Kristo. Haleluya! Roho Mtakatifu si ganda tupu, mahali ambapo watu wanaenda na . . .

208 Nalo kanisa si ganda tupu, hasa, mahali ambapo watu wanaenda, na ukumbi mkubwa wa kale, jengo, ama chochote kile, kinachogharimu dola milioni mia moja, ama chochote kile. Nasi tunatumia pesa zetu zote kwa kitu kama hicho, tunaweka mamilioni na mamilioni na mamilioni ya dola. Kanisa limefanikiwa zaidi leo hii, kifedha, kuliko lilivyopata kuwa. Lakini, tunanunua mijengo. Na hapa ninaona dhehebu kubwa

linatumia dola milioni sita, hapa Missouri, katika mahali fulani. Ambapo wao, wakati wote. . .nasi tunasema, "Kuja kwa Bwana kumekaribia," shirika la Kipentekoste. Wengine wananinii. . . Wapentekoste, wanakuja kutoka kwenye barabara ndogo, na mambo kama hayo, nao wanajaribu kujenga majengo yaliyo makubwa kuliko yote, na wapate mhubiri mwenye elimu sana wanaoweza kumleta kule.

209 Nao wanaenda mbali na kujazwa kwote na Roho Mtakatifu, wanaenda mbali na uponyaji wa Kiungu, wanaenda mbali na Roho Mtakatifu, zile Nguvu!

210 Na yote tunayofanya sasa ni kujaribu kushindana na Wamethodisti. Na sasa tumejiunga na mashirika haya makubwa ya makanisa, na kadhalika, tukikana kabisa msimamo wetu wa kiinjilisti, kwa maana tuliunda madhehebu, tukashirikishwa. Sasa wao ni wafuasi wa Baraza la Makanisa. Ni aibu jinsi gani! Ni fedheha jinsi gani, kwa kitu kama hicho! Ni huzuni jinsi gani, kukiweko na nafasi za ulimwengu unaokufa, huku ukomunisti ukiula! Na ukomunisti ulianzishwa kwa sababu ya udhaifu wa Ukristo; hiyo ni kweli, unaoitwa Ukristo.

211 Ni nafasi ya jinsi gani Kanisa la Mungu aliye hai liliyo nayo leo hii, kusimama kwa miguu yake, pamoja na ushuhuda wa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuutikisa ulimwengu huu!

212 Katika Biblia, Yeremia, mlango wa 42, walikuwa na wakati kama walio nao sasa. Waliogopa ya kwamba mfalme wa Babeli alikuwa anakuja kuwachukua. Na waheshimiwa wote, na maafisa wakubwa na kadhalika, hawakuwaamini hao manabii. Walitaka tu kusema ya kwamba waliwaamini, wapate kuwa wa kidini. Kwa hiyo wakamwita maskini Yeremia, nao walifikiri alikuwa ni mwendawazimu. Wakamtoa huko nyikani, labda amejifunika blanketi, na nywele zikining'inia usoni mwake, akila mboga, na chochote angaliweza kupata kutoka nyikani, kula. Akapanda kule, na kusema, "Nabii, tafuta kujua mapenzi ya Bwana, kwa ajili yetu." Kasema, "Twambie tutakalofanya. Nasi tutamtii Bwana, yawe mema ama mabaya."

Akasema, "Nitamtafuta Bwana kwa ajili yenu, basi."

213 Akaondoka akaenda, alikuwa ameenda kwa muda wa siku kumi kabla ya Bwana kusema naye. Akarudi, akawakusanya wote pamoja, na akasema, "Nina BWANA ASEMA HIVI." Kasema, "Sikilizeni, ninyi watu!" Haleluya! "Kwamba mnamwogopa mfalme wa Babeli," kama tunavyoiogopa Urusi. Kasema, "Mnajitayarisha kukimbilia Misri, maana mnajua yeye anakuja."

214 Nasi tunakimbia kutoka mji mmoja kwenda mwingine, tukijaribu kuzikimbia bomu za atomiki, na kujenga hifadhi na chochote kile. Zitafaa nini? Ondoeni swali la dhambi!

215 Yeremia alisema, "Kama mtamgeukia Mungu, mtoe mioyo yenu kwa Mungu, muigeuze mioyo yenu, na kuzitii Amri Zake

na maagizo Yake yote, na mfanye mambo haya yaliyo mema, basi msimwogope mfalme wa Babeli."

216 Mnajua kile watu walichosema waliposikia u—ushuhuda wa Mungu? Wao walisema, "Unatabiri uongo. Tunaenda Misri."

217 Walipofika kule chini, Yeremia alikuja akachukua mawe mawili, akayaweka kwenye shimo la matope, akasema, "Mtumishi Wangu, Mfalme Nebkadreza, atashuka aje moja kwa moja huku. Yeye ataiteka, hata hivyo! Mtakufa kwa upanga, hata hivyo."

218 Ndugu, hakuna njia kwenye siku hii, hata kidogo, kuepuka laana hii inayowangoja watu; nje ya toba ya mtindo wa kale, iliyotumwa na Roho Mtakatifu.

219 Sina kitu dhidi ya ndugu zangu. Nami ninazungumza juu ya nafsi yangu mwenyewe, lakini, sisi ni wainjilisti. Billy Graham, mwinjilisti mashuhuri; Oral Roberts, mwinjilisti mashuhuri. Hao ni watu mashuhuri. Tunawafurahia.

220 Lakini, hatuhitaji wainjilisti. Ni kitu gani? Kufanya siasa, kuunganisha makundi yote ya Kimethodisti na ya Kibaptisti na ya Kipentekoste pamoja, kushirikiana na kuonyesha jinsi tunavyoweza kuwa wakubwa, na ni wangapi tunaoweza kukusanya pamoja. Hatuhitaji jambo hilo.

221 Tunahitaji kumngojea Mungu, mpaka Roho Mtakatifu aje na Nguvu za ukombozi. Tunahitaji waokozi, si wainjilisti. Tunahitaji wokovu. "Tunaweza kuuteka mlima huu! Ni nani mlima huo mbele zetu, Zerubabeli? 'Utakuwa kama nchi tambarare,' Mungu alisema. 'Bakini nchini!'" Hiyo ni kweli.

222 Tunachohitaji leo hii ni (si uamsho) kutokea kwa wokovu, kama vile katika siku za uamsho wa Kiwelshi! Wakati watu madukani walianguka chini ya toba, wakilia, vilabu vya pombe na mahali pa anasa pakafungwa, na wakaingia kulia na kuomba, hilo ndilo tunalohitaji leo hii. Si kukusanya mia moja na hamsini elfu, kama walivyofanya hivi majuzi, baadhi yao wakisema "salamu Maria," na huyo mwingine akisema jambo lingine, ombi dogo; na wanatoka kwenda kununua pombe ya kujiburudisha, kisha wanarudi. Hiyo si siku ya maombi. Tunahitaji siku ya kulia na kuomboleza, na kungoja mpaka Mungu atakapomtuma Roho Mtakatifu, Shahidi Wake! Si ganda tupu, si dhehebu tupu; bali Mungu aliyefanyika mwili katika mwanadamu!

223 Yesu alisema, katika Marko 16, ya kwamba Roho Mtakatifu, atakapokuja, Yeye atashuhudia katika kila kizazi kifuatacho, mpaka mwisho. Alisema, "Ishara hizi! Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe; ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, katika Jina Langu watatoa pepo." Ushahidi huu utachukua muda gani? Hata mwisho wa ulimwengu! Kwa muda gani? Kila kizazi! "Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Wakishika nyoka, ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono juu ya

wagonjwa, watapata afya.” Yesu alisema ya kwamba Roho Mtakatifu ambaye angemtuma angekuwa ni Shahidi, hata mwisho wa wakati, kila kizazi baadaye.

224 Sasa, kwa kuwa Yeye alisema hivyo, sisi ni mashahidi Wake! Amina. Katika kufunga, sikilizeni kwa makini, vaeni ufahamu wenu sasa na msikilize ninapofunga. Sisi ni mashahidi Wake, ambao tumepokea Roho Wake.

225 Neno Lake linashuhudia, “Katika siku za mwisho, kwamba, utakuja ukengeufu, na utakuja wakati baridi wa kanisa, wa kawaida, usio na nguvu.” Huo ndio tunaoishi. Kanisa lisilokuwa na nguvu, “Lenye mfano wa utauwa, bali likikana Nguvu zake, hilo nalo mjiepushe nalo!” Yeye alitoa ishara, kwamba, “Kutakuwako na wakati ambapo mtu angeketi katika hekalu la Mungu, akijionyesha mwenyewe kwamba alikuwa ni Mungu. Angekuja, akiyatawala mataifa.” Ni kamilifu jinsi gani, mambo haya yote! Jinsi Neno la Mungu limekuwa kamilifu!

226 Jinsi ambavyo mfalme Nebukadreza, huko nyuma wakati alipoota hiyo ndoto, naye Danieli akamfasiria; jinsi ambavyo falme hizo, kila moja, kutoka Babeli, hata Wamedi na Waajemi, hata kwenye Wayunani, na kwa Warumi; jinsi tu walivyoanguka, tarehe ile ile, wakati, na jinsi hasa Mungu alivyosema ingekuwa.

227 Neno la Mungu ni shahidi wa kweli! Nalo Neno la Mungu lilisema, “Katika siku za mwisho zitakuja nyakati za hatari, na mioyo ya watu itavunjika kwa hofu, na mshangao wa nyakati, na dhiki kati ya mataifa. Na utakuja ule ukengeufu wa Kanisa. Na watu watainuka, na kujionyesha kwamba ni watu mashuhuri na kadhalika, nao wange—wangeondoa nguvu Kanisani; na wawe na mfano wa utauwa, na kukana Nguvu halisi za Mungu.” Kujiunga na kanisa! Yeye alinena juu ya kanisa kuingia katika hali hiyo.

228 Sisi ni shahidi ya kwamba Neno la Mungu limetimizwa. Kanisa liko katika hali hiyo, kila dhehebu liko kwenye hali iyo hiyo sasa hivi. Nita...nitampa changamoto mtu yeyote anionyeshe dhehebu lolote lililo na moto kwa ajili ya Mungu, limejazwa na Roho Mtakatifu, huku ishara zikifuatana nao. Amka uniambie moja, dhehebu lolote! Hakuna kitu kama hicho. Haliko kwenye kurasa. Hiyo ni kweli. Yote hayana nguvu na yamekufa. Yapate!

229 Bali pia Yeye alitabiri kungekuwako na Kanisa halisi katika siku hiyo, kundi dogo, masalio. Alisema kungekuwako, na kutakuwako. “Kutakuwako na watu wanaomjua Mungu wao,” alisema nabii, “watafanya mambo makuu katika siku za mwisho.”

230 Yeye alisema kungekuwako na Nuru za jioni katika siku ya mwisho. Nabii alisema hivyo! Shahidi wa kweli wa Mungu alisema hivyo, “Kutakuwako na Nuru za jioni.” Nuru ya jioni ni nini? Ni kama Nuru ya asubuhi. Nabii alisema, “Kutakuwako

na siku ambapo haitakuwa ni usiku wala mchana," wakati wa utusitusi kama ilivyo huko nje leo, nuru ya kutosha tu kuona jinsi ya kutembea hapa na pale. Lakini akasema, "Katika wakati wa jioni, itakuwa Nuru." Ingekuwa ni nini? Mngurumo, kurudi, kurudi kwenye wakati wa mwanzoni! "Kutakuwako na Nuru za jioni katika siku ya mwisho, zikiangaza."

231 Yeye alisema, "Nabii atainuka katika siku za mwisho," Malaki 4, "akitoa ishara za siku za Lutu, kadhalika, pia akiwatabiria watu warudi. 'Rudini kwenye Imani ya baba wa kwanza wa Kipentekoste! Rudini kwenye ile ya asili! Rudini kwenye Biblia! Ondokeni kwenye mashirika na madhehebu, na mrudi kwa la kwanza! Rudini kwenye pentekoste ya asili, kwenye kule kujazwa asili kwa Roho Mtakatifu, kwenye Nguvu asili za Mungu!'" Neno linashuhudia ya kwamba jambo hilo litatukia.

Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia ya utukufuni hakika mtaipata;
Katika njia ya maji, ndiko kwenye Nuru leo,
Mkizikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru za jioni zimekuja,
Ni hakika kwamba Mungu na Kristo ni mmoja.

232 Shahidi wa Mungu, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu Mwenyewe akiishi ndani yetu, asingejishirikisha katika madhehebu. Huwezi kumuundia Mungu dhehebu. Yeye ni Mungu! Litafanya nini? Litarudi jinsi lilivyokuwa hapo mwanzoni. Litarudi hapo mwanzo, litarudi kwenye mambo ya asili, litarudi mahali lilipoanzia. Litabatiza vile vile walivyofanya. Litafundisha Roho Mtakatifu vile vile lilivyofanya. Watawafundisha watu vile vile lilivyofanya. Litajiepusha na madhehebu kama vile walivyofanya. Litakuwa na nafasi kwa wote, kama walivyofanya, watakaokuja. Watakuwa safi na watakatifu kama walivyokuwa. Watajazwa na Roho Kama walivyojazwa. Watakuwa jasiri kama walivyokuwa. Na mambo yale yale yaliyowapata, yatawapata hawa katika siku za mwisho, katika Nuru za jioni, kama ilivyokuwa huko nyuma hapo awali.

Mungu, itume ile Sauti, ikaite!

233 Tuna kila namna ya mashahidi. Tuna kila namna. Tuna shahidi wa Kimethodisti, shahidi wa Kibaptisti, mashahidi wa Kipresbiteri, mashahidi wa Kikatoliki. Nitahubiri Jumapili ijayo, Bwana akipenda, juu ya hatua nne mbalimbali za kanisa, Bwana akipenda. Sasa tuna kila namna ya mashahidi leo hii, bali kuna Shahidi mmoja wa kweli.

234 Maumbile yangali yanashuhudia ya kwamba Mungu yupo. Yeye angali ni Mungu, kama alivyokuwa, mti wa

kwanza aliopata kuumba. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

235 Manabii, manabii huko nyuma, walishuhudia na walikuwa na Neno la Mungu, nao wakanena Neno la Mungu, nalo lilitimizwa moja kwa moja mbele zao. Ndipo Mungu akasema, "Akitokea mtu kati yenu, ambaye ni wa kiroho ama ni nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha kwake, katika maono, na kusema naye katika ndoto. Na kama yale asemayo yakitimia, basi msikieni."

236 Mungu yuyo huyo anafanya jambo lile lile leo hii. Tunaona jambo lile lile likitukia. Yeye alinena juu ya Nuru za jioni, zitakuja, kurudi. "Kutakuwako na mtu atakayeinuka, ambaye ataigeuza Imani ya watoto iwaelekee baba zao, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya ambayo itaiteketeza dunia kama tanuru."

237 Nasi tunaona bomu za atomiki zikining'inia huko ng'ambo. Tuliona ambapo Urusi ilifyatua lao, hivi majuzi, lenye joto na nguvu zaidi mara hamsini kuliko lile la Hiroshima. Si ajabu Japani inalilia amani, inalia na kuomba! Hiroshima, wakati lilipoyateketeza macho yao na ndimi zao, kwa umbali wa mamia ya maili, na hili walilofyatua ilikuwa ina nguvu mara hamsini zaidi. Sasa ninaona mahali ambapo cheche za mnururisho ziliikosa Marekani, zilipokuwa zikizunguka; bali wakati zitakaporudi, zitakuja juu ya Marekani tena. Cheche za mnururisho. Ngome.

238 Nawaambia, ni wakati wa kuachana, kweli, kuachana na mambo ya ulimwengu! "Utaangukia wapi, Ndugu Branham?" Kurudi mikononi mwa Mungu! Hiyo ni kweli. Hebu Roho Mtakatifu ashuhudie. Yeye ndiye Shahidi wa Mungu.

Na tuombe.

"Tutaangukia wapi, Ndugu Branham?"

239 Tunaamini jambo Hili. Tunaamini Neno ni kweli. Tunaona ya kwamba ni kweli. Tunaona ya kwamba Yeye alitabiri jambo hili katika siku za mwisho. Tunaliona. Tunaona mti Wake ukishuhudia. Tunaona maua Yake yakishuhudia. Tunaona Neno Lake likishuhudia. Tunaona Roho Wake akishuhudia.

"Tufanyeje, Ndugu Branham?"

240 Achaneni, achaneni na ulimwengu. Achaneni na mambo mliyo ndani yake. Tegemeeni tu, ninii tu . . .

"Tutaangukia wapi, Ndugu Branham?"

241 Rudini kwenye mikono ya Mungu, mseme, "Bwana, nijaze. Nijaze, Ee Bwana, na Shahidi Wako. Jalia Roho Mtakatifu awe kiongozi wangu. Jalia asininii . . . Jalia nisizunguke kila siku, nikisema, 'Vema, mimi—mimi—mimi ni Mkristo, sipaswi kufanya jambo *hili* na sipaswi kufanya *lile*.' Jalia nitiwe nguvu sana, na Roho Mtakatifu, hata nafsi yangu haiwezi kutulia."

Unasema, "Ninahofia ushupavu wa dini."

242 Kamwe usiwe na wasiwasi. Kama ukiangukia mikononi mwa Mungu, hakutakuwako na hata chembe moja ya ushupavu wa dini.

243 Katika ule uamsho wa Kiwelshi, wakati yule kiongozi mashuhuri wa uamsho wa Kiwelshi . . . Wao walimwambia, kasema, "Utakuwa na kundi la walokole."

244 Maneno pekee ambayo angeweza kusema, yalikuwa, "Tulia, na uache Roho Mtakatifu apate njia Yake; tulia, na umruhusu Roho Matakatifu." Hakuna hata chembe moja ya ulokole uliozuka. La, wote kweli walizaliwa na Roho.

245 Uamsho wa Roho Mtakatifu! Ee Mungu, utume kwa kanisa langu dogo, Baba! Utume juu ya watu hawa wanaongojea! Wakati tukiuimba ule, wimbo wa kale, Baba, mara nyingi sana:

Walikuwa katika jengo la juu,
Wote walikuwa katika moyo mmoja,
Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka
Aliyeahidiwa na Bwana wetu.

Ee Bwana, tuma Nguvu Zako sasa hivi,
Bwana, tuma Nguvu Zako sasa hivi;
Naam, Ee Bwana, tuma Nguvu Zako sasa hivi
Na kumbatiza kila mmoja.

246 Baba Mungu, kutoka kwa watoto wadogo, nina wasichana wawili na wavulana wawili humu chumbani leo, Bwana, watoto; Bwana, tuma Nguvu hizo juu yao. Wanaume wengine na wanawake wako hapa pamoja na watoto; tuma hizo Nguvu sasa hivi.

247 Akina mama wameketi hapa, na akina baba, labda kama walikuwa wanakufa leo, ingewabidi kuvuka Yo—Yordani, peke yao. Na, Ee Mungu, watakaposhuka huko, wakiukaribia ukingo huo, wakati pumzi liko karibu kuondoka, umeme unamulika, na ghadhabu ya Yehova iko juu ya mwili wenye dhambi ambao umezaliwa katika dhambi, jinsi mawimbi yatakavyopiga na umeme kuvuma, na yale mawimbi makubwa, na sehemu hatari za kina kifupi. Ee Mungu, jalia watie nanga sasa hivi katika Yesu, ili kwamba wakati huo utakapowadia, wakijua ya kwamba kuna nanga inayoshikilia, itakayowaongoza kuvuka kila shehemu hatari ya kina kifupi. Umeme au chochote kile haviwezi kuwazamisha. Wao ni salama pamoja na Yesu. Tujalie, Bwana.

248 Turehemu. Tusamehe dhambi zetu. Tujalie, Bwana. Tujaze na Roho Mtakatifu.

249 Jalia tusiridhike, Bwana, na kujiunga na kanisa na kujaribu kuwa Mkristo, kwa jitahada zetu wenyewe, njia fulani ya kujaribu kujitengenezea kitu fulani, tukisema, "Sasa ni—nimejiunga na kanisa, na watu watanitarajia kuwa Mkristo.

Na sasa haitanibidi kufanya *hili* na haitanibidi kufanya *lile* tena, kwa maana mimi ni Mkristo." Ee Mungu, jalia tuondoke kwenye hali hiyo ya Kifarisayo; Mungu, kundi hilo la wanafiki! Ee Mungu, kwa njia fulani jalia Roho Mtakatifu anene kile ninachomaanisha, Bwana. Siwezi kupata maneno ya kulisema. Hatutaki kuwa Mafarisayo wa kujifanya.

250 Mungu, tujaze na ninii yetu. . . na Uungu. Tujaze na Nguvu na uweza, mpaka nafsi zetu zitakapowaka moto, hata nguvu zetu zetakuwa ni Yeye. Ushuhuda wetu utakuwa ni Mungu. Maneno yetu yatakuwa ni Yake. Mapepo watatetemeka. Ulimwengu utatikisika na kuyumbayumba chini ya nguvu Zake, Bwana. Kama unaweza tu kuwapata watu walio tayari kumngojea Bwana!

> Wale wamngojeao Bwana, watapata nguvu mpya,
> Watapanda juu kama mbawa za tai,
> Watapiga mbio wala hawatachoka, watakwenda kwa miguu wala hawatazimia;
> Ee, nifundishe, Bwana, nifundishe, Bwana, kungoja.
>
> Nifundishe kungoja wakati mioyo inawaka moto,

Uamsho mkuu unaopitia nchini, wakisema wanawapata maelfu na maelfu, na kadhalika, Bwana; mambo makuu yenye mapambo.

> Jalia nidhalilishe kiburi changu, nikaliite Jina Lako;
> Dumisha kuifanya upya imani yangu, macho yangu yameelekezwa Kwako,
> Jalia niwe humu duniani kile unachonitaka niwe, Bwana.

251 Naomba tuiweke wakfu mitumbwi yetu midogo na minyonge, asubuhi ya leo, maskini maskani hii ya mwili huu wa aibu tunaoushughulikia sana, tunafanya kazi siku nyingi sana kuuweka kwa starehe, na tunaishi katika makazi mazuri na magari mazuri. Na, Ee Mungu, ndipo tunaelekeza macho yetu kwenye jambo hilo, na kuyaondoa kwenye u-. . . ukombozi huu mkuu. Ee Mungu, jalia tuweke kando vitu hivi vilivyolegea, tukijua ya kwamba tutaviacha hapa duniani. Na tutafute ile hazina ya Mbinguni, yule Roho Mtakatifu, yule Shahidi wa kweli wa Mungu.

252 Ufanisi kamwe haumshuhudii Mungu. Roho ndiye anayemshuhudia Mungu. Kama madhehebu yetu yanapanuka, ama kama kanisa letu linapanuka, ama kama tuna wafuasi wengi sana, ama kama tunavalia vizuri, ama kuendesha magari mazuri, ama kula chakula kizuri, hayo yanaleta tofauti gani? Hatuna budi kuuacha. Hilo lingalimfaa nini mama yangu hivi

majuzi, akisumbuka pale? Nami ninatambua, Bwana, mambo hayo hayafai kitu.

253 Jalia macho yetu yaelekezwe kwa Yesu, kwa Roho Mtakatifu, jalia aingie mioyoni mwetu na tuwe mashahidi. Jalia tuwe shahidi Wake, Bwana. Jalia tusimame katika hali hiyo, Baba, na tushuhudie.

254 Juu ya mimbara hii asubuhi ya leo, kuna leso kadhaa zimewekwa, zimetoka kwa wagonjwa na wanaoteseka. Mungu, jalia Mungu yule aliyenipa Ujumbe huu jana, jalia Mungu aliyenena kupitia kwa Ndugu Higginbotham asubuhi ya leo na kubashiri Huo ulikuwa unakuja, jalia Mungu anayeonyesha maono, anene!

255 Ninamkataa kila pepo, na kuutwaa mlima huu, kwa imani! U nani wewe, ewe mlima mkuu wa ugonjwa, unayethubutu kusimama mbele ya Bwana? Mbona, utakuwa tambarare. U nani wewe, ewe mto ama bahari ya chumvi, ambaye ungethubutu kusimama (chochote kilichokufa) mbele za Mungu? Yafungue mapito yako, tunakuja kuvuka! Tunaelekea kwenye nchi ya ahadi.

256 Ponya kila mmoja wa hawa, Bwana. Mponye kila mtu aliyeketi hapa, aliye mgonjwa.

257 U nani wewe, ewe maradhi, unafikiri wewe u nani? Shetani, unadai kwamba u nani? Kila dai ulilo nalo lilifutiliwa mbali pale Kalvari. Wewe ni mdanganyifu. Huna haki. Tunakukataa, katika Jina la Yesu Kristo; kama kundi lililojazwa na Roho Mtakatifu. Na hebu Mungu ambaye ameniongoza kote maishani mwangu, Mungu ambaye hutoa maono na kunena Maneno Yake yanayotimia, hebu Yeye, kupitia Jina la Yesu Kristo, aondolee mbali kila ugonjwa kutoka kwa watu hawa, asubuhi ya leo.

258 Ulisema, "Nena, wala usitilie shaka, bali amini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako." Ni nani aliyefanya hilo? Shahidi wa Mungu ndiye aliyesema Hilo.

259 Nami ninashuhudia asubuhi ya leo ya kwamba Neno hilo ni kweli, Shetani, kwa hiyo huna budi kuondoka.

260 Kila mtu aliye hapa ndani angeweza kuponywa sasa hivi, Nguvu za Mungu na zije juu yao, zimponye kila mtu! Imani, imani, ile—ile imani halisi; si kule kutumaini-hivyo, si kule kutenda-mema; bali Mungu yeye yule aliyelinena Neno, ashuke juu ya watu hawa! Wajaze na imani. Wajaze kwa Roho Mtakatifu. Wajaze, na uwafanye mashahidi, Bwana, ili sisi hapa pembeni tuweze kuwa shahidi Wako, shahidi kwamba Wewe u hai: Shahidi wa kweli.

261 Usiku wa leo tunakuja kwenye meza ya ushirika, kula vi—vishirikishi, visehemu vidogo vinavyouwakilisha mwili wa Bwana wetu Yesu, na kuinywa Damu Yake.

262 Mungu, isafishe mioyo yetu yenye dhambi. Ninajililia mwenyewe na kanisa hili. Sisi ni dhaifu, Bwana. Hatustahili. Sisi ni kanisa linalokiri, wala hatujajizoeza mambo tunayodai. Hatujamwacha Roho Mtakatifu atuchukue, kabisa. Sisi ni wenye dhambi. Kwa jambo hilo, tunamaanisha, Bwana, tunatilia shaka. Tunaogopa. Loo, tufanye tuzionee aibu hofu zetu za dhambi, na utujaze na ushuhuda wa Roho Mtakatifu.

263 Tuweze kuwa na Roho wa Mungu akitushughulikia sana hapa hata mamia wataketi chini ya nguvu za Mungu, wakitetemeka, wameelekeza moyo wao na upendo wao mbali na mambo ya ulimwengu, na mali yetu, tuliyo nayo. Bwana, wanafunzi hawakuijali hiyo. Waliweka . . . Waliuza yote waliyokuwa nayo na kuyaweka kwenye miguu ya mitume, wapate kuwalisha maskini. Mungu, mtume Roho Mtakatifu kwa njia hiyo, ili kwamba hatutafikiria juu ya mali tuliyo nayo, faraja uliyotupa. Tunaogopa kuteswa kidogo, ama tunaogopa tutawekwa nje, ama tutakosa usingizi kidogo, ama—ama tutakosa chakula mahali fulani. Mungu, ninakiri dhambi zangu na dhambi za kanisa langu, ninaposimama hapa, nikiyumbayumba kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

264 Jalia atende kazi juu yetu, Bwana. Nami ninaamini Yeye anatenda kazi juu yetu. Jalia tusirarue mavazi yetu. Jalia tusirarue mawazo yetu, bali tuurarue moyo wetu, tujipasue, tuyaweke wazi pale na kusema, "Mungu, mimi nina hatia. Nifinyange na unifanye, Bwana. Mimi hapa, kwenye nyumba ya Mfinyanzi. Nirarue vipandevipande, Mungu. Nitengeneze. Nifinyange. Niumbe. Kama shahi- . . . halisi wa kipentekoste."

265 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . bali Kristo na kwa Kanisa Lake. Tujalie, Ee Bwana. Ndipo ono litakuja kwenye nchi za kigeni na kokote tutakakoenda. Wagonjwa wataponywa. Wafu watafufuliwa.

266 Wala hakutakuwako na ngome ya kujihami na cheche za mnururisho tutakalohitaji. Kutakuwako na mkono wa Mungu. Kwa kuwa, kama nilivyosema hapo mwanzo wa Ujumbe, Baba, kama ambavyo uhai wa jani hurudi kwenye shina ulimotoka, na kuungojea msimu mwingine, tunajua ya kwamba tunaukaribia msimu mwingine. Tunaweza kuhisi kubadilishwa kwa mazingira, mazingira ya kiroho. Siku hiyo iko karibu kupambazuka, nasi tutaamka kwenye huo ninii mkuu . . . Utawala wa Miaka Elfu.

267 "Kwa kuwa sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia hao waliokwisha kulala mauti, kwa kuwa twasema hili kwa amri ya Bwana. Ya kwamba, baragumu italia, na hao waliolala katika Kristo watafufuka, nasi tutabadilishwa, katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho." Wakati huyo Mwana wa Mungu atakapoanza . . . Mwana wa Uzima.

268 Si zaidi ya vile unavyoweza kuificha che—chembe ya uhai, kutoka kwa jua, huo ni uhai wa mimea. Utaipenya saruji na kujitokeza. Itapenya ipate kutokea chini ya majukwaa. Itatokea mahali popote, jua litakapoanza kuangaza.

269 Si zaidi ya vile unavyoweza kuuficha Uzima wakati Uzima wa Milele unapokuja, wakati Yesu, ambaye ana Uzima wa Milele, na ni Mpaji wa Uzima wa Milele.

270 Bwana Yesu, utakapokuja, miili hii minyonge itabadilishwa katika dakika moja, na hao waliolala katika Kristo watafufuka. Nasi tutakuwa kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, ule msimu mwingine mkuu unaokuja, ule msimu wa Milele. Tubadilishe sasa, Bwana, na utuunde sasa tupate kuwa raia wa Ufalme huo.

271 Naikabidhi nafsi yangu, Bwana, pamoja na uhai uliosalia. Sijui utatuacha hapa muda mrefu kiasi gani tena, Bwana. Hakuna mmoja wetu ajuaye. Vijana wanaweza kusema, "Mimi ni mchanga," bali tunajuaje? Huenda wakaondoka kabla ya usiku. Wazee wanaweza kusema, kwamba, "Ninaondoka upesi sana," bali huenda wakaishi muda mrefu kuliko vijana. Yote yako mikononi Mwako, Bwana.

272 Bali tulicho sisi, tunakupa Wewe; nafsi yangu, nguvu zangu, moyo wangu, yangu yote. Tunajiweka wakfu, Bwana, Madhabahuni. Si kwenye madhabahu haya madogo, ya humu duniani, Bwana, bali kwenye yale Madhabahu halisi ambamo sote tunaegemea, asubuhi ya leo, tukilia kwa machozi yetu. Tunajiweka juu ya Madhabahu hayo ya Milele, na kukuomba utuchukue na kutufinyanga, na kutuunda upendavyo, na ukatufanye mashahidi. Na jalia kamwe wasisahau asubuhi ya leo, ule Ujumbe wa "shahidi wa kweli."

273 Tuna mashahidi ya kwamba tuna mabomu yaliyo bora kuliko yote ya atomiki. Tuna mashahidi ya kwamba tuna wakati wa mitambo na wakati wa kimitambo. Lakini, Bwana, ule Ufalme ujao, hakutakuwako na ndege, hakutakuwako na magari, hakutakuwako na yoyote ya mabomu haya ya atomiki. Utakuwa ni Ufalme wa amani, upendo, furaha, na uzima. Tunamwishia Yeye.

274 Yajalie mambo haya, Baba, tunapoyakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

275 Ningetaka kuuliza swali hili kabla sijaondoka. Je! mnaamini kwamba Hili ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi walio shahidi wa Roho Mtakatifu? [Wengi wanasema, "Amina."] Ni wangapi wangetaka kushuhudia Roho Mtakatifu? ["Amina."] Mungu aliyeyaandika Maneno haya, na awajalie, ndugu na dada yangu, kwamba kamwe hutapata amani nyingine humu duniani mpaka huyo Roho Mtakatifu atakapokujaza. Kwa kuwa hata kama wewe ni mfuasi wa kanisa, unapendeza, ni mzuri, ni mwema, mwaminifu, mkweli; huenda ukawa yote hayo, kisha uwe maili milioni moja kutoka kwa Mungu.

276 Yesu alisema, “Baba, siuombei ulimwengu, bali ninawaombea hawa ambao Wewe umenipa Mimi, na wote watakaoletwa nao, kwamba wapate kuutazama Utukufu niliokuwa nao pamoja na Wewe kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

277 Ndipo, kama ukija kwa huduma hii, kama ukija kwa kanisa, Yeye kamwe hakukuombea. Kama Yeye...ukija kwa dhehebu, Yeye...Maombi Yake hayana faida kwako. Bali ukija kwa ushahidi waliokuwa nao wale mitume, na wa Roho Mtakatifu, maombi Yake ni...Nawe unajua, maombi Yake, yatajibiwa. Hiyo ni kweli. Kwamba, tutashiriki, siku moja, Utukufu Wake, wa kumwona katika Utukufu aliokuwa nao kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

278 Ninaomba ya kwamba hamtapata raha, hamtaipata kamwe, mpaka mtakapompokea Roho Mtakatifu. Nami ninajiombea mwenyewe pamoja na hawa walioiinua mikono yao, walio na Roho Mtakatifu. Ninamkiri. Mnamkiri. Lakini, enyi marafiki Wakristo, tunamwacha huyo Roho Mtakatifu akae bwete. Tuna—tunazishughulikia sana a—anasa za maisha. Tunaogopa mateso madogo. Tunayaogopa mambo haya. Na tuuweke ulimwengu huu kando.

> Msiutamani utajiri wa bure wa ulimwengu huu,
> Ambao huoza upesi sana,
> Tujenge matumaini yetu juu ya mambo ya Milele,
> Hayatapita kamwe.
>
> Ushikilie mkono wa Mungu usiobadilika!
> Ushikilie mkono wa Mungu usiobadilika!
> Unapoachwa na marafiki wa duniani,
> Shikilia tu karibu zaidi na Yeye!

279 Mshikilie. Hebu sisi, kama Wakristo wanaodai Roho Mtakatifu, na tujionee aibu sana, na tuudhike sana katika roho yetu, hata hatutaacha mpaka tuwe taa zilizo hai, zinazowaka, tuliojazwa Roho, na kumruhusu afanye kazi kupitia sisi. Simaanishi katika kundi la ulokole. Mnajua vema zaidi ya hayo. Ninamaanisha katika njia ya kweli ya Mungu, yenye uchaji, kwa ubatizo wa Roho, kwa nguvu na dhihirisho, tupate kutenda kazi katika siku hizi za mwisho, tukijua kwamba mwisho umekaribia.

280 Mungu awabariki. Mmekuwa waaminifu sasa kuketi hapa muda mrefu, mpaka, kwa saa yangu, ni karibu saa sita na dakika kumi na mbili. Labda imechelewa zaidi ya hapo. Bali hata iwe nini, asanteni kwa usikivu wenu mkamilifu. Ombi langu, baraka zangu na ziwe pamoja na kila mmoja wenu. Na—nawapenda.

281 Mmethibitisha kwamba ninyi ni rafiki yangu. Nilipokuwa mhitaji, mlionyesha kwamba ninyi ni rafiki yangu. Hapo ndipo

rafiki halisi huonyesha kama ni rafiki. Mlithibitisha kwamba ninyi ni rafiki yangu.

282 Na, enyi marafiki, huenda nikasema mambo magumu na mambo ya kukatakata, kutoka hapa. Labda mnafikiri nililidharau shirika lenu ama dhehebu. Sikulimaanisha kwa mwelekeo huo. Ninamaanisha tu hivi: kuwa rafiki yako, sina budi kuwa mkweli. Sina budi kuwa mwaminifu.

283 Kama nikikuona ukishuka mtoni, katika mtumbwi mdogo, nami ninajua maporomoko yako tu kule chini, huo mtumbwi hauwezi kuyaabiri mawimbi hayo. Hauwezi kuyaabiri. Ungezama. Na kama nikikupigia makelele, "Toka kwenye mtumbwi huo." Si kwamba ninakuchukia. Ninakupenda. Ninajaribu tu kuyaokoa maisha yako.

284 Na hivyo ndivyo ninavyosema asubuhi ya leo, ninapoyasema mambo haya. Ninayasema kwa stahamala ya upendo na ushirika. Enyi marafiki, hata kama sisi ni Wapentekoste, tunahitaji kutikiswa, hata kama sisi ni Wabaptisti, ama Wamethodisti, ama chochote tulicho, chapa hizo za kanisa.

285 Kama nilivyomwambia Bw. Coots, mwenye kuzika. Yeye alisema, "Billy. . . " Alikuwa akizungumza juu ya mahubiri, na kadhalika. Naye ni . . . yeye daima huja. Yeye ni Mkatoliki. Nafikiri ndivyo alivyo mkewe. Na—naamini ndivyo alivyo, pia. Hata hivyo, yeye daima huja na kunisikiliza nikihubiri. Naye hushuka kuja wakati ninapoanza kuomba, angeingia ndani, asimame humu, nasi tulikuwa tukilizungumzia pale nje. Akasema, "Daima ninapenda kukusikiliza, Billy." Nikasema, "Bw. Coots, chapa kamwe haiubadilishi ukoo wa ng'ombe."

286 Kama chapa ilikuwa juu ya herefodi, alikuwa ni herefodi, kwanza kabisa. Mnaona? Chapa haiubadilishi ukoo.

287 Kwa hiyo kama wewe ni Mmethodisti ama Mbaptisti, ama wewe ni wa Umoja ama Uwili, ama kundi lolote la Kipentekoste unaloshiriki, loo, ndugu yangu, chapa yako kamwe haibadilishi kile ulicho. Huenda ukaitwa Mpentekoste, upigwe chapa hiyo, bali kama wewe si mptentekoste moyoni, rohoni, wewe si mpentekoste. Chapa hiyo ni ya kupania tu, ya kukupoteza.

288 Maskini ng'ombe wa kawaida wa shambani anaweza kuvaa chapa nzuri, bali hiyo haifai kitu. Huenda akavaa chapa ya herefodi, bali yeye si herefodi.

289 Wewe ni Mkristo unapojazwa; na hakuna njia nyingine yoyote. Hakuna kanuni za imani, hakuna dhehebu unaloweza kujiunga nalo, hakuna sala unazoweza kukariri; yote ni bure. Huna budi kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, la sivyo umepotea. "Mtu asipozaliwa mara ya pili, kamwe hatamwona Mungu." Hiyo ni kweli. Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Na kuzaliwa mara ya pili, huna budi kujazwa na Roho Mtakatifu, nguvu za Mungu. Mungu! Huna budi kuyafungua maisha yako na kujitupa nje, na kuuruhusu Uungu, Mungu, ajifanyie mwili ndani yako.

Hiyo ni Kweli, ndugu yangu, dada. Mungu na atusaidie sisi sote kumpokea, ndilo ombi langu.

Ndugu Teddy, *Peleka Jina La Yesu.*

290 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ati nini? [Mtu fulani anazungumza tena na Ndugu Branham.]

291 Billy anataka nitangaze ya kwamba hatawatumia ninyi watu kadi juma hili ambao mlitaka kuhudhuria mikutano, ya juma lijalo, kwa kuwa tayari imetangazwa.

292 Mnampenda Bwana? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa moyo wenu wote? ["Amina."] Mtainua mikono yenu, kuahidi hilo? [Kusanyiko linaomba kwa sauti pamoja na Ndugu Branham.] "Mungu, nisaidie. Nisaidie, Ee Mungu, kulipeleka Jina la Yesu. Jalia niliishi Jina la Yesu. Jalia nimwone, katika amani. Jalia nimwalike moyoni mwangu. Jalia aje ndani yangu. Nijalie, tangu leo hii, Bwana, kuwa Wako kabisa."

293 Tunaahidi hili, Bwana, Kwako, kama watu, baada ya ujumbe huu; kwamba, haidhuru ni dhehebu lipi, ni mhemko upi, tumefanya nini: kama tumepaza sauti, kama tumepiga mayowe, kama tumenena kwa lugha, kama tumecheza katika Roho, ama yoyote ya mihemko hii. Ee Mungu, jalia Roho Mtakatifu alilete ndani ya mioyo ya watu sasa, kujua ya kwamba mambo hayo hayana maana. Kwamba, ni kuufanyia Uungu maskani, Mungu, mioyoni mwetu. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Yesu, ya kwamba utatufinyanga na kutufanya tufanane na mapenzi Yako. Amina.

> Tunaliinamia Jina la Yesu,
> Tukisujudu miguuni Pake,
> Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme,
> Safari yetu itakapokamilika.
>
> Jina la thamani,

Sasa peaneni mikono mmoja na mwingine.

> . . . ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha za Mbinguni,
> Jina la thamani . . .

[Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]

294 Ninataka kufanya tangazo lingine. Nilisahau, sikujua hilo, hasa. Kuna ibada ya ubatizo, unaoifuata hii. Kama mtu yeyote hapa, ambaye hajabatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, hebu nikwambie, kama mtumishi wa Mungu, ubatizo ni muhimu kwa wokovu. "Aaminiye na kubatizwa," na kubatizwa, "ataokolewa." Sasa, kama hujabatizwa katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo, nawe umemwamini Yeye na kukiri dhambi zako, njoo mbele sasa baada ya ibada hii nawe unaweza kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zako.

295 Kumbukeni, Mathayo ilisema, "Enendeni basi, mkayafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu" ni sifa ambazo ni za Jina la Yesu Kristo. Kanisa lote la mwanzoni lilibatiza, mpaka kule kuzaliwa kwa kanisa Katoliki, wote walibatiza katika Jina la Yesu Kristo. Hebu chukua *Baraza la Nikea*, *Wale Wazee*, na kadhalika, vya historia, nawe utaona, lakini basi walianza kutumia sifa badala ya Jina. Sisi kama kanisa, kundi la watu, sio dhehebu, tunabaki na Biblia. Ni Jina la Yesu Kristo. Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego;
Majaribu yakikuzungu-. . .

Sikilizeni. Unafanya nini wakati majaribu?

Litaje Jina hilo katika maombi.

Jina la thamani (Jina la thamani), Ee jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha za Mbinguni;
Jina la thamani, jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha za Mbinguni.

296 Tuviinamishe vichwa vyetu sasa. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Peleka Jina La Yesu*—Mh.]

Tukisujudu miguuni Pake,
Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa wafalme, (lini?)
Safari yetu itakapokamilika.
Jina la thamani . . .

Ndugu Neville.

*Ushuhuda Wa Shahidi Wa Kweli* SWA61-1105
(The Testimony Of A True Witness)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 5 Novemba, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org